

**KUCHUNGUZA DHAMIRA VUATE ZINAZOIBUKA KATIKA METHALI
ZA KIPEMBA**

KHATIB HAJI MAKAME

**TASINIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUTIMIZA SEHEMU YA
MASHARTI YA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UMAHIRI YA KISWAHILI
(M.A KISWAHILI) KATIKA IDARA YA LUGHA NA TAALUMA ZA
FASIHI YA CHUO KIKUU HURIA CHATANZANIA**

2023

UTHIBITISHO

Aliyeweka saini hapa chini anathibitisha kuwa ameisoma Tasnifu hii iitwayo *Kuchunguza Dhamira Vuate zinazoibuka katika Methali za Kipemba* na kupendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa ajili ya kukamilisha masharti ya kutunukiwa shahada ya Uzamili ya Kiswahili (M.A Kiswahili) katika Idara ya Luga na Taaluma za Fasihi ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

DKT. MOHAMED OMARY MAGUO

(**Msimamizi**)

Tarehe_____

TAMKO

Mimi **Khatib Haji Makame** nathibitisha kwamba tasinifu hii ni kazi yangu halisi na kwamba hajjawahi kuwasilishwakatika Chuo Kikuu kingine kwa ajili ya kutunukiwa shahada ya uzamili ya Kiswahili au shahada ya aina nyengine yoyote.

Sahihi

Tarehe

HAKI MILIKI

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhuswi kuiga au kunakili kwa njia yoyote ile, iwe ama kazi nzima au sehemu ya tasnifu hii, isipokuwa kwa shughuli halali, kwa ajili ya utafiti, kujisomea, au kufanya marejeo ya kitaaluma bila kibali cha maandishi cha mtafiti au Mkuu wa Kurugenzi ya Taaluma za Uzamili kwa niaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania

SHUKRANI

Kwanza kabisa ni jukumu langu kubwa kumshukuru Allah (SW) kwa kunipa uhai na kuniwezesha kuifanikisha kuifanikisha kazi hii nzito hadi kuifikisha tamati. Ni kwa uwezo wake ulilifanya kila jambo lililokamilika likamilike kwa nguvu na utashi wake.

Pili napenda kumtakia rehema na baraka za ziada Mtume wetu Muhammad (S. A W) yeýé mwenyewe binafsi na familia yake yote pamoja na umma wake wote.

Tatu napenda kumshukuru kwa dhati msimamizi wangumwalimu Bakari Kombo Bakari kwa kuweza kunipatia kila aina ya msaada hadi nikaweza kuitamatisha kazi hii, yenye kuhitaji juhudhi na maarifa ya kiwango cha juu. Mwalimu Bakari hakuwa msimamizi tu, bali alikuwa ni muelekezaji aliyetumia upole na hekemima kubwa za kukosoa na kushauri.

Nne, nawashukuru wazazi wangu kwa kunipatia kila aina ya msaada na kuweza kunifariji kwa pale ninapopambana na changamoto mbali mbali hadi kuifikisha mwisho tasnifu hii. Wazazi walininasahi na kunipa moyo wa kupambana na kuyafanya mawazo yao kuwa ni chachu zilizonisaidia kutatua changa moto hizi na zile.

Aidha, napenda niitumie nafasi hii kwa kumshukuru mke wangu mpendwa Ziada Farhan Khamis kwa kunipa moyo hadi nikaweza kuikifisha tamati tasnifu hii. Nawashukuru pia watoto wangu kwa uvumilivu wao wa kunistahamilia na kukubali

kukosa haki zao walizostahiki kuzipata kwa kipindi chote nilipokuwa masomoni,
hasa katika kufanya utafiti na kuitayarisha ripoti hii.

Mwisho napenda kuwashukuru walimu wangu wote walionifundisha kuanzi elimu ya
msingi, sekondari, hadi elimu ya juu zaidi.

TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa wazazi wangu walionilea na kuniingiza kwenye elimu ya msingi ambayo imekuwa ndio chachu na ngazi ya kupandia juu hadi kufikia hatua hii ambayo leo hii nimefika.

IKISIRI

Utafiti huu ulilenga “*Kuchunguza Dhamira Vuate zinazoibuka katika Methali za Kipemba.*” Utafiti huu ulifanyika maktabani na uwandani katika ukusanyaji wa data. Maeneo yaliyotumika kukusanya data ni katika shule za sekondari za Vitongoji, Dkt. Omar, Utaani na Mchangamdogo. Maeneo haya yalitumika kukusanya data kwa kutumia hojaji. Maeneo mengine yaliyotumika kupata data za Mahojiano ni Wawi na Vitongoji. Sampuli ya utafiti huu iliteuliwa kwa kutumia mbinu ya madhumuni maalum. Aidha, data za utafiti huu zilichambuliwa kwa kutumia mbinu ya maelezo. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji na Nadharia ya Simiotiki. Jumla ya Methali thelathini na tano za jamii ya Wapemba zilichambuliwa kutoka kwa watafitiwa waliojaza dodoso na wale waliohojiwa kwenye eneo la utafiti. Data zilifanyiwa uchambuzi na uwasilishaji kwa njia ya maelezo. Utafiti huu uliongozwa na malengo mahususi mawili ambayo ni; “Kubainisha methali mahususi za jamii ya Wapemba.” Lengo hili liliongozwa na swali la utafiti lisemalo “Ni methali zipi mahususi za jamii ya Wapemba?” Lengo mahsusla pili la utafiti huu lilikuwa ni: “Kubainisha Dhamira Vuate zinzojitokeza katika methali za jamii ya Wapemba”. Lengo hili liliongozwa na swali la utafiti lisemalo “Ni dhamira zipi zilizovuatwa katika methali za jamii ya Wapemba?” Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa, methali za Kipemba hugawanyika kwenye matapo mbalimbali. Zipo methali zinazohusu Nyanja za kijamii, kiuchumi, kisiaza, kimapenzi na hata kiutamaduni. Baadhi ya methali za Kipemba huvuata dhamira moja na nyengine huvuata dhamira zaidi ya moja.

Maneno Makuu: *Kuvuata, Kipemba, Dhamira*

YALITYOMO

UTHIBITISHO	ii
TAMKO	iii
HAKI MILIKI.....	iv
SHUKRANI.....	v
TABARUKU	vii
IKISIRI	viii
YALITYOMO	ix
ORODHA YA JEDWALI	xiii

SURA YA KWANZA: UTANGULIZI 1

1.1 Utangulizi	1
1.2 Usuli wa Mada.....	1
1.3 Tatizo la Utafiti.....	5
1.4 Lengo la Utafiti.....	7
1.4.1 Lengo Kuu	7
1.4.2 Malengo Mahususi	7
1.5 Maswali ya Utafiti	7
1.6 Umuhimu wa Utafiti.....	8
1.7 Mipaka ya Utafiti.....	8
1.8 Mpango wa Utafiti	9

SURA YA PILI: MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA

KINADHARIA 10

2.1 Utangulizi	10
----------------------	----

2.2	Ufafanuzi wa Dhana ya Methali.....	10
2.2.1	Lugha katika Methali.....	13
2.2.2	Dhana ya Dhamira.....	13
2.3	Dhima za Fasihi	14
2.4	Tafiti kuhusu Methali	15
2.5	Pengo la Utafiti.....	23
2.6	Mkabala wa Nadharia.....	23
2.6.1	Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji	24
2.6.2	Nadharia ya Simiotiki.....	27
2.6.2.1	Misimbo ya Nadharia ya Simiotiki.....	28
2.7	Hitimisho	30
	SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI	31
3.1	Utangulizi	31
3.2	Eneo la Utafiti.....	31
3.3	Kundi Lengwa	31
3.4	Sampuli na Usampulishaji.....	32
3.4.1	Sampuli.....	32
3.4.2	Usampulishaji	32
3.5	Ukusanyaji wa Data.....	33
3.5.1	Data za Msingi.....	33
3.5.2	Data za Upili.....	33
3.6	Mbinu ya Kukusanya Data	34
3.6.1	Mbinu ya Hojaji.....	34

3.6.2	Usaili.....	35
3.7	Usahihi, Kuaminika na Maadili ya Utafiti	35
3.7.1	Usahihi wa Data	35
3.7.2	Kuaminika kwa Data za Utafiti	36
3.7.3	Maadili ya Utafiti	36
3.8	Hitimisho	37

SURA YA NNE: KUBAINISHA METHALI MAHUSUSI ZA JAMII YA

	KIPEMBA	38
4.1	Utangulizi	38
4.2	Methali zinazoakisi Maudhui za Kijamii	38
4.2.1	Methali zinazoakisi Maudhui za Kiuchumi.....	39
4.2.2	Methali zinazoakisi Maudhui za Kisiasa.....	39
4.2.3	Methali zinazoakisi Maudhui za Kimapenzi	40
4.2.4	Methali zinazoakisi Maudhui za Kiutamaduni	40
4.3	Uchambuzi wa Dhamira Vuate wa Methali za Jamii ya Kipemba.....	41
4.3.1	Utangulizi	41
4.3.2	Dhamira Vuate Ndani ya Methali zenyne Maudhui ya Kijamii	41
4.3.3	Dhamira Vuate Ndani ya Methali zenyne Maudhui za Kiuchumi	49
4.3.4	Dhamira Vuate Ndani ya Methali zenyne Maudhui ya Kisiasa	57
4.3.5	Dhamira Vuate Ndani ya Methali zenyne Maudhui ya Kimapenzi	69
4.3.6	Dhamira Vuate Ndani ya Methali zenyne Maudhui ya Utamaduni	76
4.4	Hitimisho	79

SURA YA TANO: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO	80
5.1 Utangulizi	80
5.2 Muhutasari wa Tasinifu.....	80
5.3 Matokeo ya Utafiti.....	82
5.3.1 Lengo Mahususi la Kwanza	82
5.3.2 Lengo Mahsusni la Pili	82
5.4 Hitimisho	83
5.5 Mapendekezo ya Utafiti	83
5.5.1 Mapendekezo kwa Watafiti.....	83
5.5.2 Mapendekezo kwaWakuza Mitaala.....	84
5.5.3 Mapendekezo kwa Waandishi wa Vitabu	84
MAREJELEO.....	85

ORODHA YA JEDWALI

Jadwali Na. 1: Sampuli ya Utafiti 32

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.1 Utangulizi

Sehemu hii inashughulikia vipengele vya kiutangulizi vya utafiti huu. Vipengele ambavyo vimebainishwa katika sehemu hii ni usuli wa mada ya utafiti, tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti na mipaka ya utafiti. Kimsingi sehemu hii inalengo la kufanya ufanuzi juu ya vipengele vya msingi vya kiutangulizi katika kazi yoyote ya utafiti.

1.2 Usuli wa Mada

Mada ya utafiti huu inahusu kipengele kimoja miuongoni mwa vipengele muhimu sana vya semi. Semi zimekilita katika utanzu mmoja wapo miuongoni mwa tanzu mama za fasihi simulizi. Kwa muktadha huu mtafiti hana budi kuangazia ingawa kwa ufupi kuhusu fasihi simulizi. Matteru (2003), anasema kuwa fasihi simulizi ni aina ya sanaa itumiayo maneno ya mdomo katika mpangilio na maumbo mbalimbali kutoa dhana ama mawazo fulani. Kwa maana nyengine ni kwamba utumizi wa lugha na maneno yaliyomo katika lugha, kisanii, huunda sanaa ya fasihi. Fasihi simulizi, ikiwa ni sanaa itumiayo maneno katika kutoa dhana fulani, hutegemea sana nyenzo mbalimbali za kuonekana na kusikika zitumiwazo na binadamu katika kujieleza.

Fasihi simulizi imegawika katika tanzu mbalimbali ambazo huweza kuekwa katika vigawanyo vitatu ambavyo ni tanzu za kinathari, kishairi na semi (Matteru, 2003). Uainishaji huu unakinanza na ule unaofanywa na Mulokozi (1996), ambapo anazitaja tanzu za fasihi simulizi kama vile semi, mazungumzo, masimulizi, maigizo, ushairi na ngomezi. Mawazo haya ni muhimu sana katika kuzibainisha tanzu za fasihi

simulizi. Hata hivyo, ngomezi kama inavyobainishwa na Mulokozi kwamba ni utanzu wa fasihi simulizi ni suala linalohitaji mjadala. Hii ni kwa sababu ngomezi si matumizi ya lugha ilhali fasihi ni matumizi ya lugha ya kisanii.

Matumizi ya lugha ya kisanii katika fasihi huweza kujikita katika tungo za kinahau, misemo, tamathali za semi na methali. Kwa sababu lengo kuu la utafiti huu limejikita kuchunguza dhamira chomokezi katika methali, basi kwanza ni vema mtafiti akaeleza maana ya methali kama mbinu ya matumizi ya lugha katika kazi za fasihi.

Ndungo na Mwai (1991), wanasma kwamba methali ni semi fupi au kauli ambazo huwa na maana nzito au hekima ndani yake. Kauli hizi huwa zenyenye busara na mafunzo kuhusu maisha na mahusiano ya watu. Methali hutumia lugha ya mkato ya kuonya au kusisitiza jambo fulani. Wanaendelea kusema kuwa methali zahitaji ujuzi wa kuzifafanua kwa sababu maana zake huwa zimefichwa na mara nyingi huwa ni mafumbo. Methali hutumiwa kumjuvya mtu ukweli fulani au kumshitunga ili apate kudadisi mambo au kujisahihisha anapokosa.

Ndungo na Mwai (wameshatajwa), wanasema kuwa dhima kuu ya methali hujitokeza katika malezi. Hii ni kwasababu methali huwa zimejaa maadili ambayo humsaidia mwanadamu kumuongoza kwenye msingi bora wa maisha. Zinaweza kuwa za masuto au mawaidha. Metahali za mawaidha ni zile zenyenye lengo la kuonya, kuusia, kushauri na kufunza. Methali za masuto huwa na lengo hilohilo lakini maneno yake ni ya kukaripia na hata kukemea. Maneno ya aina hiyo mara nyingi hayatumiki katika halaiki au mbele ya watu wazima au wageni. Katika maelezo haya tunajifunza kwamba dhamira kuu ya methali hujikita katika malezi ya vijana. Hata hivyo kwa

uzoefu wa mtafiti anaona kwamba methali hazijikiti tu katika malezi bali hujikita katika nyanja zote za maisha ya wanajamii kama vile siasa, uchumi na utamaduni.

Kuhusu fani ya methali hasa katika matumizi ya lugha Wamitila (2010), na Ndungo na Mwai (1991), wanasema methali hutumia lugha ya kitamathali au yenyе kujenga picha. Kwa kawaida picha hizo huwa zimebeba ujumbe ambaо umefichika. Pia, ili kuzielewa baadhi ya methali lazima kuzihusisha na na miktadha lakini zipo methali ambazo huweza kueleweka bila ya kuzihusisha na muktadha moja kwa moja. Wamitila (ameshatajwa), anasema kuwa sifa kuu inayotambuliwa na wana paremolojia ni kwamba methali huwa na wingi hali na wingi dhamira. Methali moja huweza kutumika kueleza hali tafauti na dhamira zake huweza kuwa nydingi sana.

Watafiti kadhaa wamewahi kufanya uchunguzi unaohusu utanze wa semi ikiwemo methali. Mathalani, Maitara (2012), aliandika makala yenyе anuani `Uainishaji wa Ushairi kwa kutumia Kigezo cha Methali. Katika mjadala wake anaeleza kuwa maana inayokusudiwa katika methali huweza kubainishwa zaidi kupitia muktadha mahususi unaoibuliwa au kwa kupatanishwa na ujumbe unaowasilishwa. Kwa hivyo ufasiri hutegemea jinsi mtunzi alivyoufumba ujumbe na jinsi mpokezi anavyolikabili shairi hilo tangu mwanzo; mradi tu aweze kuthibitishia hoja zake kwa mifano dhahiri inayotokana na miktadha halisi katika utamaduni wa jamii. Mawazo haya yanatupa uelewa kwamba methali hazitumiki kiholela bali hutumika kutegemea muktadha ili kuibua dhamira zilizokusudiwa.

Naye Mayoka (1977), aliandika makala yenyе mada `*Fasili ya Methali*.` Katika makala hiyo Mayoka anamawazo ambayo yanakinzana na mtazamo ya baadhi ya

wataalamu wengine kwa namna fualani. Mathalani, Maitara (2012), anatiliamkazo muktadha katika ufasiri wa methali lakini Mayoka anatilia mkazo suala la kuelewa utamaduni wa jamii husika. Anasema kwamba methali zetu nyingi hueleweka kutokana na chimbuko la tamaduni zetu. Wageni wetu watokao nje ya mandhari ya maisha yetu huwa vigumu kuzielewa kwani hisia nyingi tuzipatazo, wao hawazipati.

Khamis (1983) anaendelea kueleza kwamba manyanyaso na dharau hizo zilitokana na sababu ya kwanza, tangu kale fasihi simulizi ilihuishiwa na watu wasiojua kitu, wajinga wasiojua kusoma na kuandika, na ambao hawakuweza kufarajika kwa kazi walizozifanya. Pili, hata wakati huu ustarabu wa kibepari ndio unaofaa kwamba ndio uliofuta fasihi ya kishenzi. Tatu fasihi simulizi imevizwa kwa maendeleo ya kiufundi na uvumbuzi wa mashine kadhaa, hasa uchapaji na za mawasiliano kama vile redio, tepurikoda na televisheni. Kwa namna hii inaonekana hakuna haja ya kushughulika na fasihi simulizi kwa sababu wakati wake umepita. Hata hivyo, Khamis (1983), anapinga vikali mawazo hayo na anaona kuwa fasihi simulizi ni chombo cha maendeleo. Anasema hivi:

Tanzania ni mionganoni mwa nchi ambazo angalau zimetaja nia ya kujenga ujamaa. Kwa hivyo, mbali na siasa yake ya kufufua, kulinda kuhuisha yale ya jadi yaliyo mnasaba na amali za ujamaa, imeamua kuitumia fasihi simulizi kwa madhumuni ya kuifanya iwe ni chombo cha maendeleo` (uk. 4).

Maelezo haya yanatupatia uelewa kwamba fasihi simulizi ina umuhimu mkubwa katika jamii. Na kutokana na umuhimu huo Tanzania ni mionganoni mwa nchi za bara la Afrika ambayo inathamini fasihi simulizi. Haja iliopo kwa wakati tulionao ni kuendelea kuthamini fasihi yetu na kuendeleza tafiti mbalimbali kuhusu fasihi simulizi.

Jambo lililomsukuma mtafiti kuwa na shauku ya kutaka kufanya utafiti huu ni baada ya kutalii machapisho mbalimbali ambayo yanahu fasihi simulizi. Katika utalii huo alisoma makala ya Khamis (1983), yenye anuani '*Nafasi ya Fasihi Simuizi katika Jamii ya Kitanzania*'. Katika makala hiyo anaeleza kuwa manyanyaso ambayo yamekuwa yakitupiwa fasih simulizi hayakuanza leo, yanarudi nyuma toka enzi za kitumwa za Plato na Athens na hata katika wakati wa kimwinyi na kikabila huko ulaya.

Kutokana na utalii alioufanya mtafiti hakuona kazi ya utafiti yoyote iliyowahi kufanyika ikiwa na lengo la kuchunguza dhamira chomokezi katika methali za jamii ya Wapemba. Kwa mantiki hiyo mtafiti anaona iponafasi ya kufanya utafiti huu ili kuchunguza dhamira chomokezi katika jamii ya Wapemba.

1.3 Tatizo la Utafiti

Kuna kazi kadha zilizofanywa kuhusu methali za Kiswahili na Lugha nyengine duniani. Miongoni mwa kazi za Kiswahili zilizoichambua stadi ya methali ni zile za Oniango (1978), Mulokozi (1996), Mbiti (1996), Chacha (1999) Mphande (2001), Wamitila (2001), Nkwera (2003), Senzighe (2004), Mauya (2006), Alzarock (2016) na Sheha (2019). Kazi iliyofanywa kwamawanda mapana zaidi ni ile ya Mauya (2006) na Wamitila (2001). Wamitila (keshatajwa) aliandika kamusi ambayo imekusanya methali za Kiswahili zaidi ya 2,000 ambazo ni mkusanyo mpana kabisa wa methali za Kiswahili uliowahi kuonekana mpaka sasa. Wamitila (keshatajwa) katika kamusi lake hili ameingiza methali za aina mbalimbali kama vile zisikikavyo katika jamii nyingi za Waswahili katika upwa wa Afrika Mashariki na kwengineko ambako lugha ya Kiswahili inatumika na kuzungumzwa. Mauya (2006) kwa upande

wake amezikusanya zaidi ya methali 300 na kuziweka katika makundi kama 59 hivi. Makundi haya bwana Mauya (keshatajwa) aliyaanisha katika miktadha mbalimbali. Mauya (keshatajwa) hafafanui tu usemi na maana yake, bali pia anauhusisha na maisha halisi kwa kutumia mifano hai, na anaorodhesha methali nyingine zenye kufanana na kila methali.

Nkwera (1999) kwa upande wake anaeleza maana ya methali na nafasi yake katika fasihi kwenye *Tamrini za Fasihi Simulizi*. Anatoa vipengele vitatu vya uhakiki wa methali ambavyo ni maana ya maneno yasimamavyo, ufanuzi wa fumbo au mfano uliotumika, na maadili ya methali. Baada ya hapo, Nkwera anatoa mifano kadhaa ya uchambuzi wa methali. Pia anapanga makundi manane ya methali. Mwishowe, Nkwera anachambua matumizi na sanaa katika methali.

Nyangwine na Masebo (2008) anazungumzia mbinu za kisanaa katika methali, kama vile sitiari, kejeli, msisitizo, ukinzano, tashhis. Halkadhalika Nyangwine na Masebo (weshatajwa) anatoa taswira katika methali: taswira za wanyama, za ndege, za samani, na za matunda.

Pamoja na jitihada zote zilizofanywa na watafiti walijotajwa hapo juu, mtafiti hajabaini kazi yoyote iliyochunguza.

Kazi zilizofanywa zimejeribu kueleza kwa kiwango fulani mambo yanayohusu, lugha iliyotumika katika methali na kuchambua vipengele mbalimbali vya matumizi ya lugha kama vile matumizi ya tamathali za semi na miundo ya methali. Kwa upande wa dhamira watafiti waligusia dhamira zilizojitokeza katika methali za jamii

mbalimbali. Dhamira katika methali za jamii hizo ni pamoja na dhamira za malezi, kuwajibika katika kazi, kupendana, kuimarisha umoja na mshikamamo katika kuwasaidia wengine kwa shida na raha na ukandamizaji wa jinsia ya kike na kuimarisha mfumo dume. Pamoja na jitihada hizi dhamira zilizo ndani ya methali za jamii za Kipemba bado hazijaangaziwa kwa jicho angavu la kiutafiti. Kwa mantiki hii mtafiti wa kazi hii ameamua kufanya utafiti kuhusiana na mada iliyohusuKuchunguza Dhamira Vuaye zinzoibuka katika Methali za Kipemba ili kupunguza mwanya ulioachwa na watangulizi wake.

1.4 Lengo la Utafiti

Utafiti huu una lengo kuu na malengo mahususi kama yafuatayo:

1.4.1 Lengo Kuu

Lengo kuu la utafiti huu ni kubainisha dhamira chomokezi zinazojitokeza katika methali za jamii ya Wapemba.

1.4.2 Malengo Mahususi

Malengo mahususi ya utafiti huu ni:

- i. Kubainisha methali mahususi za jamii ya Wapemba
- ii. Kubainisha dhamira vuaye zinazojitokeza katika methali za jamii ya Wapemba.

1.5 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu utaongozwa na maswali ya utafiti yafuatayo:-

- i. Ni methali zipi methali za jamii ya Wapemba?
- ii. Ni dhamira zipi zilizovuatwa katika methali za jamii ya Wapemba?

1.6 Umuhimu wa Utafiti

Kukamilika kwa utafiti huu kunatarijiwa kuwa na umuhimumkubwa katika vipengele muhimun vifuatavyo:-

Kitaaluma: Matokeo ya utafiti huu yanatarajiwakuwa marejeleo muhimu kwa wasomi wa ngazi zote za taaluma ya fasihi. Wanafunzi, walimu na wasomi wengine wa kazi za fasihi wanatarajiwa yatumia matokeo ya utafiti huu kama ni sehemu ya marejeleo yao ya kukamilisha malengo na madhumuni ya tafiti watakazozifanya baadae. Pia, matokeo ya utafiti huu yatatumika kama sehemu ya kujiimarisha, ili kubainisha pengo la maarifa ambalo baadhi ya watafitiwa watalijaza kupitiatafiti zaowatakazokusudia kufanya.

Katika taaluma ya fasihi: Utafiti huu utatoa mchango mkubwa katika uwanja wa fasihi simulizi na kuonesha dhamira mbalimbali zinazojitokeza kupitia methali za jamii ya Wapemba.

Kiutamaduni: Kwa vile utafiti huu umehusu dhamira chomokezi katika methali jamii ya Wapemba na vipengele vya lugha ni matumaini ya mtafiti kwamba methali za jamii ya Wapemba zitakuwa zimekusanywa na kuekwa pamoja. Kufanya hivyo, utafiti utakuwa umetunza historia ya jamii. Pia, kupitia dhamira chomokeza zitazobainishwa kwenye methali za Wapemba zitasawiri utamaduni wa Wapemba. Hii ni kwa sababu fasihi ni zao la jamii husika.

1.7 Mipaka ya Utafiti

Jamii ya Wapemba imekuwa ikitumia vipengele kadhaa vya lugha katika maisha yao ya kila siku. Vipengele hivyo ni pamoja na nahau, methali, taswira na tamathali za

semi. Kwa sabau vipengele hivi ni vingi mno katika jamii hiyo haitakuwa rahisi kuvitafiti vipengele vyote hivyo vya lugha kwa wakati mmoja. Kwa hivyo, mtafiti ameamua kutafiti dhamira chomokezi zinazojitokeza katika methali za jamii ya Wapemba. Kufanya hivyo anaamini kwamba atajibu maswali ya utafiti huu.

1.8 Mpango wa Utafiti

Utafiti huu utakuwa wa uwandani. Data zimekusanywa uwandani zitalenga kwenye utanzu wa methali, hasa za zinazotumiwa na jamii ya Wapemba. Utafiti huu utatumia mkabala wa kimaelezo na kitarakimu katika kuchambua na kuwasilisha data za utafiti.

SURA YA PILI

MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA

2.1 Utangulizi

Pons (1992), alibainisha kuwa utalii wa kazi tangulizi huhusisha kupitia nyaraka, usomaji wa machapisho yaliyoandikwa ambayo mtafiti huyapitia kwa kuyasoma ili kupata taarifa anazozitafuta kulingana na mada na malengo yake ya utafiti. Hivyo mtafitiwa kazi hii ametaliikwa kinamachapisho kama vile, majarida na vitabu ili kupata data za utafiti wake anazozihitaji. Pia kutalii ni namna ya usomaji unaofanywa umakini kwa lengo la kupekua taaluma iliyojificha. Kwa msingi huo, mtafiti wa kazi hii alilazimika kusoma vitabu, majarida, tasnifu za watafiti waliomtangulia, pamoja na kusoma mitandaoni ili kufichua siri za watafiti tangulizi na kupata maarifa zaidi na kurahisishaufanyaji na uandishiwa utafiti wake.

Katika kufanikisha malengo ya utafiti huu, mtafiti wa kazi hii alifanya mapitio ya maandiko yaliyogawanywa katika makundi makuu matano. Kwanza, ni mapitio yanayozungumzia dhana mbalimbali. Pili ni mapitio yanayohusu utafiti wa methali. Tatu, mtafiti amebainisha pengo la utafiti. Mwisho wa sehemu hii tumefanya ufanuzi wa nadharia ya Simiotiki na Mwitiko wa Msomaji ambazo ndizo zilizoongoza utafiti wetu.

2.2 Ufanuzi wa Dhana ya Methali

Methali ni semi fupi fupi zinazoshehenifumbo na fumbizi za aina mbalimbali juu ya ukweli wa maisha ya binadamu na mara nyingi huwa na umbo maalum lenye muundo wa kimafumbo. Simiyu (2013) ameeleza kwamba mafumbo yanayojenga

methali huwa yanalenga kufikisha ukweli bila ya kuwakwaza walengwa. Methali ni aina ya misemo ambayo huwa na pande mbili, upande wa kwanza huwa ni kama swalii na upande wa pili huwa ni majibu ya swalii lililoulizwa. Kwa lugha nyengine mtafiti anaweza kusema kwamba, methali nyingi huwa na muundo wenyewe sehemu mbili, sehemu ya kwanza huanzisha wazo fulani na sehemu ya pili hulikamilisha au kulikanusha wazo lenyewe. TUKI (2004) inaeleza kuwa methali ni usemi wa kisanii wa kimapokeo unaofikiriwa na jamii kuwa kweli na unaotumiwa kufumbia au kupigia mfano. Ufafanuzi kama huu pia umewahi kutolewa na Ndalu na King'ei (1988) ambao wanasema kwamba methali ni usemi wenyewe fumbo lenye falsafa nzito lenye utata na mguso wa jamii ambao ni msemo wenyewe ukale uliorithishwa kutoka kizazi kimoja hadi chengine. Utanzu wa methali hutegemea sana unategemea sana fani nyingine ili uweze kukua na kuenea. Mfano, methali inaweza kuibuka ili kutilia mkazo hoja fulani iliyobuka kwenye maongezi au majadiliano mazito. Kwa muktadha huo inaonekana kwamba, methali ni kipera elekezi ambacho hutumiwa kufafanua na kukazia hoja juu ya jambo linalozungumzwa ili lieleweke vizuri. Mara nyingi muundo au mtindo wa methali huwa wa kishairi. Mbonde (2005) amekuja na maoni yasemayo kwamba methali ni njia ya mkato ya kuelimisha, kuadilisha, kukosoa na kueelekeza jamii hususani vijana katika kuzingatia tunu za jadi kwa kina ndani ya mazingira ya uasili ya jamii. Mulokozi (1996) anafafanua kuwa methali ni semi fupi zenyе kuelezea kwa muhtasari fikra au mafunzo mazito yaliyotokana na uzoefu wa kijamii. Mara nyingi mawazo hayo huelezwa kwa kutumia tamathali hasa sitiari na mafumbo. Methali ni maneno ya hekima na busara ambayo hutolewa na mtu mmoja na baadaye maana ya maneno hutolewa. Jambo la msingi katika kutoa maana ama fasili ya methali ni kuangalia mazingira. TUKI (1981) Inafafanua kuwa, Methali

ni kifungu cha maneno yanayotumiwa pamoja kisanii kwa njia ya kufumba au kupigia mfano na ambacho kinachukua maana ndefu na pana kuliko maneno yenyewe yanayotumiwa; muhtasari wa maneno ya kisanii wenyewe maana pana. (Ndalu 1997) yeche anaona kwa methali ni sehemu ya semi kwenye kijipera cha msemu. Methali daima inakuwa ni misemo ya kimapokeo ambayo ina muundo fulani mahsusini unaokumbukika na unaokusudiwa, kuelezeza, kuadhibu, kusuta, kulaumu na kushauri. Inapotolewa maana ya methali ni muhimu kuzingatia kwa undani muktadha wa matumizi ya methali wenyewe.

Mlacha (1981) amekuja na madai yasemayo kwamba methali kwa uhakika ni mkusanyiko wa mambo mengi: Amebainisha na kutaja mambo hayo kuwa ni ujuzi wa lugha, shuhuda za vitendo, matukio mbalimbali, hekima kubwa. Ngole na Honero (1981) wao wanaeleza kuwa methali ni aina moja ya usemi mzito na ambao unakusudiwa kusema jambo maalum lakini kwa namna ya fumbo. Kinachosemwa katika methali mara nyingi huwa kinakusudiwa kuwa ni onyo, lililotolewa kwa lengo la kumuongoza na kumwadibisha mwanadamu.

Wakisitisiza juu ya umbile na muundo wake wa nje (Ngole na Honero, 1981). Wanaeleza kwamba methali huwa na muundo maalum. Muundo wenyewe unakuwa na pande mbili. Upande wa awali wa methali hii, huwa unaeleza mazoea au tabia ya mtu au kitu juu ya utekelezaji wa jambo na upande wa pili huwa unaeleza matokeo yatokananyo na mazoea hayo ambayo imeelezwa upande wa kwanza.

Kwa ujumla mtafiti anajumuisha mjadala wa dhana ya methali, kwa kusema kwamba methali ni usemi mfupi wenyewe maana pana na busara au hekima ulio na mizizi katika

jamii fulani na unaoelimisha, kuasa au kukejeli watu au vitendo fulani katika jamii lakini kwa njia iliyofumbwa na kuwekewa tafsida. Kila jamii ina methali zake za aina tofauti tofauti kuambatana na utamaduni na mila zilizomo katika jamii hiyo. Kwa upande mwingine methali hubadilika na nyingine mpya kuibuka kuambatana na mabadiliko ya jamii inayohusika.

2.2.1 Lughya katika Methali

Mayoka (1977) anaeleza kuwa, lughya ya methali huwa na mpango maalumu wa maneno yaliyopangiliwa vito vya hekima ambayo kwazo mtu huweza kupata kitabu kizima cha mafundisho. Maneno ndani ya methali huvutia sana na kushawishi akili kuyakariri. Ili kupata maana sadifu ya methali ni lazima mtu aweze kufafanua maneno yote yalivyotumiwa katia vipengele vyake vyote. Methali mara kwa mara hutumia tamathali za lughya katika kueleza mambo ya dunia yanayojiri. Hutumia tashbiha na sitiari katika kuonesha mshabaha wa vitu.

2.2.2 Dhanya ya Dhamira

Wamitila (2002), anasema kwamba dhamira ni istilahi ya kifasihi inayotumiwa kurjelea mada ya kazi fulani, ujumbe au lengo la kazi hiyo. Anaendelea kusema kuwa dhamira ni ile jumla ya maana anayoivumbua mwandishi aandikapo kazi ya fasihi na jumla ya maana anayoivumbua msomaji katika usomaji wake. Uvumbuaji wa maana hiyo huweza kufanyika kwa kuisoma kazi hiyo kwa kina, msomaji akielewa visehemu mbalimbali pamoja na jinsi visehemu hivyo vinavyohusiana na kazi nzima na kuibuka na kitu kimoja. Maana hii ni nzuri katika kueleza dhanya ya dhamira. Hata hivyo mapungufu makubwa yanajitokeza katika kile mtafiti anachoweza kukiita ‘utengo.’ Utengo huo umejitokeza kutokana na Wamitila

kujikita katika fasihi andishi na kutoihusisha fasihi simulizi ambayo haimo katika mfumo wa maandishi. Hivyo basi, tunachoweza kusema hapa ni kwamba dhamira huweza kujitokeza hata kwenye fasihi ya kimasimulizi pia.

Maelezo haya ya Mulokozi (1996), Mieder na Litovikna (1999) na Mieder (2007), yanatupatia uelewa wa maana ya methali kwamba ni kipengele cha lugha ambacho kinatokana na utanze wa semi na huweza kutambulika kwa kuwa na pande mbili. Upande wa kwanza hutegemea upande wa pili. Pia, tumebaini kuwa baadhi ya methali huweza kuwa na mapigo ya kishairi. Hivyo mawazo haya yatamsaidia mtafiti katika kuzibainisha methali za jamii ya Wapemba.

2.3 Dhima za Fasihi

Ndungo na Mwai (1991) na Ndungo na Wafula (1993), wameibuka na maoni yasemayo kwamba, tunaposhughulikia dhima ya asihi simulizi tuna maana ya kuzungumzia jukumu kubwa linalofanywa na fasihi hii. Na dhima ina maana wajibu mkubwa wa kufanya jambo, madaraka au wadhifa. Fasihi ni chombo muhimu sana katika jamii na kama chombo chawenza kutumiawa kwa shari au kwa heri kulingana na matakwa au mtazamo wa msanii. Inaweza kutumiwa kuwachonga wanajamii ili wayaangale mazingira yao kwa udadisi na uchambuzi ili waweze kujikosoa na kujirekebisha.

Vile vile fasihi katika jamii ya kitabaka yaweza kutumiwa na tabaka fulani kuwapotosha au kuwapumbaza wanajamii wasiweze kuangalia mazingira yao kwa jicho la upembuzi wa kina na hapo wasiweze kuona chanzo cha maovu yanayowakumba katika jamii.

Ndungo na Mwai (1991), wanamnukuu Plekano (1957), ambapo anaeleza kuwa kuna misimamo miwili kuhusu fasihi na jamii. Msimamo wa kwanza ni ule unaodai kuwa fasihi ni chombo kimoja wapo katika harakati dhidi ya mazinngira. Msimamo huu unasisitiza kuwa sanaa inapasa kusaidia kumuamsha mwanadamu ili apambane na mazingira machafu. Mtazamo wa pili ni ule wa wanasanaa wanaosisitiza kuwa kufanya sanaa kama chombo ni kukidunisha na kukidhalilisha. Wanadai kwamba sanaa ni lengo na wala si chombo.

Kwa ujumla katika utafiti huu mtafiti anaungana na mawazo ya Ndungo na Mwai (1991), ambao wanahitimisha mjadala huu kwa kusema kuwa iwapo fasihi ina faida kwa wanajamii haina budi kuwa chombo kiaminifu cha jamii hiyo. Ni lazima iwe na wadhifa wa kuchambua, kukosoa na kuiongoza jamii katika kuleta mabadiliko ambayo yatakuwa na manufaa kwa wanajamii wote.

2.4 Tafiti kuhusu Methali

Utalii uliofanywa na mtafiti katika machapisho mbalimbali ulibaini kuwa wapo watafiti wengi waliovahidi kutafiti kipera cha methali. Baadhi ya tafiti zilizofanywa zimejikita kuchunguza Methali za lugha ya Kiswahili na nyengine zikiwa na lengo la kuchunguza methali katika lugha nyengine za Kiafrika. Baadhi ya tafiti hizo ni kama zifuatazo:

Methali katika jamii ya Watanzania bado ni kipengele ambacho hakijafanyiwa utafiti wa kutosha ikilinganishwa na kazi nyingine za fasihi zilivyodiriki kuandikiwa. Sababu za jambo hili bado hazijulikani. Mtafiti anafikiri sababu za kuwepo hali hiyo ni zile alizozitaja Wamitila (2008) ambazo ni kwamba wataalamu wengi hudhani

kuwa methali hazina mambo mengi ambayo yanaweza kufanyiwa utafiti. Hata hivyo, wapo wataalamu wa Kitanzania ambao wamediriki kuchunguza juu ya methali za jamii mbalimbali za Tanzania. Miogoni mwa wataalamu hao ni kama vile Chacha (1999) ambaye alikusanya methali za jamii ya Wakurya wanaoishi mkoani Mara na kuzifanya uchambuzi. Katika uchambuzi wake aligundua kwamba methali za jamii ya Wakurya zina utajiri mwangi wa vipengele vya dhamira. Miogoni mwa dhamira alizoziona ni zile zinazohusu, malezi, kuwajibika katika kufanya kazi, kuimarisha umoja na mshikamano, kupendana na kusaidiana katika shida na raha.

Kazi ya Chacha (keshatajwa) ni ya masilahi makubwa sana kwa mtafiti wa kazi hii, kwa sababu mtafiti wa kazi hii mbali ya kwamba hachunguzi dhamira za methali za Wakurya, lakini kwa kuwa mada yake inahusiana na kuangazia dhamira chomokezi za methali za jamii ya Kipemba, inaonekana kuwepo uwiano wa karibu kati ya utafiti wa Chacha (keshatajwa) na utafiti huu. Hivyo utafiti wa Chacha (keshatajwa) utakuwa ni dira na mwelekeo mzuri utakao muongoza mtafiti wa kazi hii kuibua dhamira chomokezi za methali za jamii ya Kipemba.

Mwenerwa (2003) ana maoni kwamba, maendeleo ya Sayansi na teknolojia yana mchango mkubwa katika kudidimiza methali za makabila ya Tanzania kuliko mchango wa kuendeleza na kudumisha methali hizo. Mwanataluma huyu anaeleza kuwa teknolojia imechangia sana kudunisha methali za jamii ya Wahaya ambapo Wahaya huziona methali zao kama kitu kilichopitwa na wakati. Hii inatokana na watu wengi kukimbilia kudhamini kazi za fasihi ambazo zinaoneshwa katika televisheni na mitandao ya kijamii na kuzibakisha nyuma methali kama kwamba hazipo kabisa katika jamii yao. Baadhi ya Wahaya huzichukulia methali kama vitu

vya utamaduni wa kizamani sana vilivyoitwa na wakoloni kuwa ni vya kishenzi. Mawazo ya (Mwenerwa 2003) ni thabiti na ni ya kweli tupu kwani hivi sasa katika jamii nyingi za Kiafrika methali zimesahaulika na kushushwa thamani yake. Hili ndilo jambo ambalo limemsukuma mtafiti wa kazi hii kufanya utafiti huu ili pamoja na malengo mengine aweze kukusanya na kuchambua methali za jamii ya Wapemba kwa lengo la kuibua dhamira chomokezi zitakazoonyesha umuhimu wa methali katika jamii za Watanzania, Pemba ikiwemo.

Senzighe (2004) yeye alitafiti methali za jamii ya Wapare katika kipengele cha jinsia. Senzighe (keshatajwa) alibaini kwamba methali za Wapare zinaikandamiza jinsia ya kike. Katika methali za Kipare kwa mujibu wake mwanamke anasawiriwa kama kiumbe dhaifu asiye uwezo wa kutoa mawazo mazuri ya kupeleka mbele jamii yake na badala yake huwa ni msikilizaji tu wa yale yanayosemwa na wanaume. Hii ina maana kuwa, mwanamke hapewi nafasi ya kushiriki katika maamuzi muhimu yanayofanyika katika jamii yake na hivyo yale mambo ambayo yanamlenga moja kwa moja kama mwanamke yanakosa kupatiwa masuluhisho muafaka. Mawazo ya Senzighe ni ya kweli na yanajitokeza katika methali za jamii nyingi duniani kutokana na kutawala kwa mfumo dume uliopo katika jamii. Mfumo dume humfadhilisha mwanaume na kumuona kuwa ndiye mwenye akili na maarifa ya kuweza kutoa maamuzi sahihi juu ya masuala yahusuyo familia na hata taifa. Mawazo haya ya Senzighe (keshatajwa) yatakuwa ni kioo kitakachomiwezesha mtafiti katika upembuzi wake wa dhamira kuangazia iwapo Wapemba wana ubaguzi wa kijinsia au jambo hilo halikujitokeza.

Bwanamaya (2004) alifanya utafiti uliochunguza uhusiano uliopo baina ya mabadiliko katika jamii na methali katika jamii ya Wakerewe. Matokeo ya utafiti wake yalionesha kuwa mabadiliko yanayotokea katika jamii hususani kutokana na kuingiliana kwa jamii moja na nyingine kuna changia sana kupotea kwa methali katika jamii ya Wakerewe. Wakerewe walipokuwa wakiishi peke yao bila maingiliano na jamii nyingine za Tanzania walikuwa wakitumia methali zao kwa kiasi kikubwa kama chombo cha kufundisha mema na kukataza mambo mabaya katika jamii yao. Hivi sasa jamii ya Wakerewe inaishi pamoja na mchanganyiko wa jamii nyingi na hivyo matumizi ya lugha ya Kikerewe na methali zake ni ndogo sana. Mabadiliko kama haya yanaonekana kuzikumba jamii nyingi za Watanzani, jamii ya Waswahili wa Pemba ikiwa ni mojawapo. Kazi hii ni ya manufaa makubwa kwa mtafiti wa kazi hii kwani itamuwezesha kubaini iwapo methali za Wapemba zinaimarika au kudumaa kwa maingiliano ya Wapemba na jamii mbalimbali wanazotangamana nazo.

Madumulla (2005) amefanya utafiti katika kabile la Wahehe, ametafiti methali za kihehe na kubaini kuwa kuna methali za kihehe zinazohusisha ndege, vifo, uwindaji, Mungu, miti, maisha, wadudu, wanawake, wanaume, wachawi na hata magonjwa. Katika maelezo yake anabainisha kuwa, pamoja kwamba kuna methali kama alivyozigawanya katika makundi haya lakini methali zote zipo kwa ajili ya kutoa elimu ya kumfundisha binadamu namna bora ya kuweza kuishi na wanadamu wengine. Kazi ya Madumula (keshatajwa) itakuwa ni dira njema ya kuangazia hasa methali za Wapemba zimehusisha picha za aina gani na zimeibua dhamira gani chomokezi.

Kwa upande wa lugha ya Kiswahili zipo pia kazi chache zilizoandikiwa na kufanyiwa utafiti. Miongoni mwa kazi za Kiswahili zilizoichambua stadi ya methali kwamawanda mapana zaid ni ile ya Mauya (2006) na Wamitila (2001). Wamitila (keshatajwa) aliandika kamusi ambayo imekusanya methali za Kiswahili zaidi ya 2,000 ambazo ni mkusanyo mpana kabisa wa methali za Kiswahili uliowahi kuonekana mpaka sasa. Wamitila (keshatajwa) katika kamusi lake hili ameingiza methali za aina mbalimbali kama vile zisikikavyo katika jamii nyingi za Waswahili katika upwa wa Afrika Mashariki na kwengineko ambako lugha ya Kiswahili inatumika na kuzungumzwa. Miongoni mwa methali alizoingiza Wamitila (keshatajwa) ni zile zilizopatikana katika tafiti mbalimbali Uswahilini. Amezinyokoa kotuka kwenye tafiti za Mombasa, Lamu, Unguja na Dar es Salaam. Katika uchambuzi wake huu Wamitila ametoa maana ya ndani na muktadha wa matumizi ya kila methali. Mauya (2006) kwa upande wake amezikusanya zaidi ya methali 300 na kuziweka katika makundi kama 59 hivi. Makundi haya bwana Mauya (keshatajwa) aliyaanisha katika miktadha mbalimbali. Mauya (keshatajwa) hafafanui tu usemi na maana yake, bali pia anauhusisha na maisha halisi kwa kutumia mifano hai, na anaorodhesha methali nyingine zenye kufanana na kila methali. Kazi ya Wamitila (keshatajwa) na Mauya (keshatajwa) inatarajiwa kutoa mchango mkubwa kabisa kwa mtafiti wa kazi hii. Maana za kimuktadha zilizotolewa na wawili hawa zinatarajiwa kutoa mwanga mkali utakaommurikia mtafiti wa kazi hii ili kujua kwamba kiini cha methali ni kwa ajili ya kuibua maana ya kimuktadha zaidi kuliko kuibua maana itokanayo na vijenzi vyta methali inayohusika. Jambo hili litamuwezesha mtafiti kuzichunguza maana za kimuktadha na jinsi zitakavyoibua dhamira chomokezi zitokanazo na methali za jamii ya Wapemba.

Nkwera (1999) kwa upande wake anaeleza maana ya methali na nafasi yake katika fasihi kwenye *Tamrini za Fasihi Simulizi*. Anatoa vipengele vitatu vya uhakiki wa methali ambavyo ni maana ya maneno yasimamavyo, ufanuzi wa fumbo au mfano uliotumika, na maadili ya methali. Baada ya hapo, Nkwera anatoa mifano kadhaa ya uchambuzi wa methali. Pia anapanga makundi manane ya methali. Mwishowe, Nkwera anachambua matumizi na sanaa katika methali. Kazi ya Nkwera (keshatajwa) imekuwa ni ya manufaa makubwa kwa mtafiti wa kazi hii, kwani mtafiti amepata mwanga ungaruzao kwa uangavu mkubwa unaomuonesha ni jinsi gani dhamira zinaweza kuibuka. Kwanza Nkwera (keshatajwa) ameanza kuchambua methali kwa kuangalia maneno yasimamayo kuijenga methali wenyewe. Pili amefumbua mafumbo au mfano uliotumika na mwisho kutoa maadili ya methali. Kwa kuongozwa na kusaidiwa na nadharia teule mtafiti wa kazi hii ameainisha kupitia mtazamo wa Nkwera dhamira za methali kama zilivyojichomoza katika methali za jamii ya Wapemba.

Nyangwine na Masebo (2008) wanazungumzia mbinu za kisanaa katika methali, kama vile sitiari, kejeli, msisitizo, ukinzano, tashhisi. Halkadhalika Nyangwine na Masebo (weshatajwa) wanatoa taswira katika methali: taswira za wanyama, za ndege, za samani, na za matunda. Nyangwine na Masebo (weshatajwa) hatoi mifano mingi katika kila sehemu, lakini hata hivyo kazi ya Nyangwine inaweza kuwa ni chanzo kizuri kinachoweza kumfanya mtafiti kutafuta mifano zaidi kufuatana na mantiki aliyokusudia kuichambua.

Kazi ya Nyangwine na Masebo (weshatajwa) ni ya msaada wa kiasi fulani kwa mtafiti. Kuainisha kwake taswira katika methali kunampa mtafiti mwanga wa awali

wa kufikiria jinsi atakavyotumia nadharia yake ya Simiotiki katika kuibua dhamira chomokezi za methali teule za jamii ya Wapemba. Tofauti kubwa iliyopo kati ya kazi hii na maandiko ya Nyangwine na Masebo (weshatajwa) ni kwamba Nyangwine na Masebo walikuwa wanawasilisha methali kama kijipera cha fasihi zimulizi, ilhali mtafiti wa kazi hii anaiangazia methali kama chombo kilichobeba dhamira pana katika muktadha wa kijamii.

Maitaria (2013), aliandika kazi yenyewe kichwa cha habari “Matumizi ya Methali katika Ushairi wa Shaaban Robert.” Katika makala hayo Maitaria (keshatajwa) anaeleza kuwa methali ni zao la utamaduni wa jamii, matumizi yake yameuweka ushairi katika mkabala wa uhalisi wa maisha ya watu. Kupitia kwa methali, tungo za ushairi wa Kiswahili zinakuwa kanzi ya kuhifadhia na kubainishia falsafa ya mtunzi kuhusu maisha. Kadhalika, ujumbe unaowasilishwa hueleweka kwa tafakuri kubwa zaidi kuhusu masuala mbalimbali yanayoihusu jamii. Kwa maana hiyo, mtunzi amejenga dira ya kuwaelekeza wanajamii katika kukabiliana na matatizo katika jamii ya sasa. Vile vile, methali hizo zinawasilisha mawazo muhimu yanayothibitiwa nautamaduni wa jamii. Katika muktadha huo, ushairi wa Shaaban Robert umeshughulikia nyanja muhimu katika maisha ya watu.

Kazi ya Maitaria ingawa ilijikita kuchunguza methalia katika ushairi lakini itakuwa na umuhimu mkubwa katika utafiti huu. Kwanza, kazi hiyo ilionesha namna matumizi ya methali yanavyotumika kutegemea miktadha ya kijamii. Pili, kazi hiyo inaonesha namna methali zinavyoweza kugawika katika matapo mawili kutegemea ufumbuaji wa maana. Kundi la kwanza ni lile la methali ambazo maana zake ni ngumu kuzifumbua, na kundi la pili ni la methali ambazo ni

maana zake ni rahisi kuzfumbua. Umuhimu wa pili wa kazi hii ni kwamba umemuonesha namna mtafiti anavyoweza kufumbua maana za methali kutegemeana na muktadha wa matumizi kwenye miktadha kadha wa kadha.

Nao Mulokozi na Kitogo (2007), walikusanya methali zilizowahi kutumiwa na Shaaban Robert katika maandishi yake. Methali hizi ziko katika orodha tu ya chapisho la mumbukumbu za methali za Shaaban Robert kama bingwa wa fasihi ya Kiswahili. Kazi ya Mulokozi na Kitogo (weshatajwa) ingawa haikuonesha kwa undani matumizi ya methali hizo kimaana na kimiktadha. Hata hivyo, mtafiti amebaini metahali na miundo yake. Kazi hii itamsaidia mtafiti kuona jinsi methali za Kiswahili zinavyokusanywa na kurikodiwa kwenye kumbukumbu na kwa hivyo itakuwa rahisi kuzikusanya methali za jamii ya Wapemba na kuziweka katika orodha katika mpangilio unaofaa.

Pia, Msuya (1977) aliandika makala yenyenye anuani *Fasili ya Methali*. Katika makala hiyo alieleza namna lugha ya methali inavyotumika katia kufikiasha ujumbe kwa jamii. Katika uchambuzi huo Msuya anaonesha namna methali zilivyo kiungo muhmu katika kufikisha ujumbe kwa jamii. Pia, anatanabahisha kwamba methali huwa na maana zilizo wazi na zilizofichika. Hivyo katika kuzielewa methali lazima mchambuzi azingatie miktadha ya matumizi ya methali na muktadha husika. Anatoa mfano wa methali inayosema ‘Akili nyingi huondoa maarifa.’ Katika kuifanyia uchambuzi methali hii Msuya (ameshatajwa) anasema kuwa mawazo tunayoyapata ni kwamba bila akili binadamu angebaki kiumbe dhalili ajabu. Mambo mengi yaliyonayo sasa katika uwezo wake asingeyamdu. Akili ndio nyenzo kuu ya maisha ya binadamu. Bila kutumia nyenzo hii kazi nyingi ngumu zisingefanyika. Basi kwa

nyenzo hii ndio maana tunatekeleza kazi nyingi. Hivyo methali hii hupigiwa watu ambao hujitia werevu wakupindukia. Watu wengine hujifanya kuwa wanajua kila kitu na hivyo basi hawataki kusahihishwa wala kufundishwa. Ndio maana hupigiwa vijembe kuwa ‘akili nyingi huondoa maarifa.’ Kazi ya Msuya imekuwa ya manufaa makubwa kwa mtafiti wa kazi hii kwa kuwa imetoa muongozo wa jinsi muktadha wa methali unavyoweza kusaidia uibukaji wa dhamira fiche zilizokusudiwa ambazo zinaendana moja kwa moja na mada ya mtafiti wa kazi hii.

2.5 Pengo la Utafiti

Mtafiti wa kazi hii amesoma kazi nyingi za watangulizi wake na amegundua vipengele kadha vinavyohusu matumizi ya lugha na dhamira tofauti za methali. Dhamira mbalimbali zilichambuliwa katika methali za jamii mbalimbali na kuonyesha vipengele tofauti vya dhamira zilizojitokeza. Methali za Kipemba ambazo ndizo zinazokusudiwa kuangaziwa dhamira zake inaonekana bado hazijatafitiwa kwa kiwango cha kutosha. Kwa hivyo mtafiti wa kazi hii alikusudia kufanya utafiti wa kuchunguza dhamiri vuate zinazoibuka katika methali za Kipemba ili naye aweze kutoa mchango wake wa kitaaluma.

2.6 Mkabala wa Nadharia

Utafiti huu utaongozwa na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji na Simiotiki. Nadharia hizi zimeteuliwa na mtafiti akiamini kwamba zina misingi imara ambayo itawezesha kuwasilisha data za utafiti huu kwa misingi ya kisayansi. Mtafiti ametumia nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ili kutoa maoni yake binafsi kwa kiasi anavyoilewa jamii iliyomzunguka. Simiotiki imetumika ili kufumbua mafumbo na fumbizi zilizoficha dhamira mbalimbali ambazo ndizo zenye kubeba kiini cha utafiti huu. Nadharia zote

mbili zimetumika kuchambua lengo la pili kutegemeana na haja iliyojitokeza. Hivyo, nadharia ya Mwitiko wa Msomaji imefanyiwa uwasilishaji kama ifuatavyo:

2.6.1 Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji

Wafula na Njogu (2007) wanasema nadharia ya Mwitiko wa Msomaji iliasisiwa na James na wenzake katika miaka ya 1960-1970. Waasisi hawa ni Wajerumani ambao wanaamini kuwa kazi ya fasihi inapaswa kutazamwa kwa kulingana na mila, desturi na utamaduni wa msomaji. Kwani msomaji ana uhuru wa kutafsiri kama aonavyo kutokana na uzowefu wake, na si kutokana na uzowefu wa mtunzi. Wanaendelea kueleza kuwa wanadadharia hawa wanaweza kuwekwa katika matapo matatu ambayo ni:

- Wale wanaoangazia kwenye tajriba za kipekee za msomaji. Hawa ni pamoja na C. C. Lewis, (1961), Stanley Fish (1967), na Normana Holland (1968), ambao walikuwa Wamarekani.
- Wale wanaofanya majaribio ya kisaikolojia kwa kikundi maalumu cha wasomaji. Hawa ni Reuven Tsur, Richard Gerring, David Miell na Donald Kuiken
- Wale wanaochukulia kwamba wasomaji wote wa kazi ya fasihi wataipokea kwa njia iliyosawa.

Hata hivyo, Wafula na Njogu (2007) wanasema kuwa Stanley Fish anadai kwamba sanaa ya maneno haichanganuliwi kwa kutumia mikakati ya jaribio la kisayansi. Anayefanya jaribio la kisayansi huweka mpaka wa kihisia na kimawazo kati ya nafsi yake na jambo linalomshughulisha.

Wananadharia hao wanaeleza kuwa kazi ya fasihi inajikita katika ishara na taswira.

Kutokana na ishara na taswira hizo matini za kifasihi huwa hazina maana moja bali zinakuwa na maana zaidi ya moja. Msingi mkuu wa nadharia hii ni kwamba kazi yoyote yahuuliza maswali ambayo kwayo misingi ya nadharia hii imejiegemeza.

Maswali hayo ni kama haya yafuatayo:

- Kuna uwiano wowote kati ya maana inayosomwa na jinsi msomaji anavyoihakiki?
- Je, kila kazi ya fasihi ina maana kufuatana na msomaji binafsi na namna anavyoichukulia?
- Kuna wasomaji ambao husoma na kufasiri kazi za fasihi vizuri zaidi kuliko wasomaji wengine.
- Msomaji hutumia vigezo gani kujijulisha iwapo mawazo yake juu ya kazi fualani yanafaa au hayafai?

Kwa upande mwngine Wafula na Njogu (2007) wanasema kwamba Kinoti (2012) anamnukuu Adena Rosmarin katika Murfin (1999) ambaye anaeleza kwamba kazi ya fasihi ni kama kinyago ambacho hakijakamilika na kwa hivyo mchongaji hujaribu kukikamilisha. Kwa hivyo, Kinoti anaibainisha mihimili ya Mwitiko wa Msomaji kama ifuatayo:

- Msomaji huikamilisha kazi ya sanaa kwa kuijaliza kwa usomaji makini au kwa kuidhalilisha kwa usomaji wa kiholela. Iser na Fish wanadai kwamba kazi ya fasihi huwa na mapengo mengi ambayo msomaji hushurutika kutunga matini mpya amabazo zimechochewa na kuzalika kutokana na matini asili zilizoko kwenye kurasa.

- Nadharia hii inasisitiza athari za kazi za fasihi juu ya akili na maarifa ya mwandishi. Wasomaji hufasiri athari hizo kuitia njia tofauti toafauti kutegemea:
- Tofauti kati ya matini na hisia za kibinaksi za msomaji.
- Namna matini inavyoelekeza au kutatiza mwitiko wa msomaji. Sifa ianyozua usomaji mzuri ama mbaya wa kazi ya fasihi.
- Wanana dharia hii wanashikilia kuwa kuna njia mbili za usomaji wa kazi za fasihi ambazo ni:
- Njia inayofafanua na kusisitiza mawazo ambayo kitambo yamejuilikana na kutambuliwa na msomaji.
- Kuwasilisha kazi ya fasihi kimafumbo ili kumchochea msomaji kujitafutia na kujamulia ujumbe uliomo katika kazi aliyoisoma. Kwa hivyo, mafumbo hayo yanapaswa kusomwa na msomaji mara kadhaa ili kupata ujumbe uliokusudiwa.
- Usomaji ni tendo linalofanywa na kutekelezwa na msomaji kwa wakati maalumu, kwamba wakati wa kusomwa kwa matini huathiri maana ya matini hiyo.
- Msomaji anyetumia nadharia ya Mwitiko wa Msomaji hufuata hatua tatu, ambazo ni:
- Hurejelea kazi inayosomwa kwa tafsiri ili ithibitishwe kwamba kazi hiyo inaafikiana nay ale yanayokumbukwa na msomaji.
- Hubainisha jinsi miktadha ya matini isiyohusiana moja kwa moja na maandishi inavyoweza kuhsishwa na kutangamanishwa na msomaji.

- Hudhihirisha kwamba maoni ya msomaji yanafungamana na mada muhimu za hadithi.
- Nadharia hii inazingatia usomaji, msomaji na upokezi.

Mapungufu ya Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji

Nadharia hii imekuwa ikikosolewa na baadhi ya wahakiki kwa sababu ya mtazamo kuwa inapokuwa kwa mtunzi huwa haina maana mahususi. Kwa mfano, Salim (2015) anasema kwamba nadharia ya Mwitiko wa Msomaji inaelezwa kuwa na mapungufu kutokana na kuiona kazi ya fasihi kutokuwa na maana mpaka pale inapoingia mikononi mwa msomaji. Kwa mantiki hiyo, msomaji asiyekuwa makini anaweza kuipa kazi husika maana finyu. Pamoja na mapungufu haya bado mtafiti aliona kuwa inaweza kuwa muafaka katika kufikia malengo yanayohusu dhamira katika soga za vijiweni. Hivyo mtafiti aliitumia nadharia hii na kufikia lengo la kwanza na utafiti huu.

2.6.2 Nadharia ya Simiotiki

Wamitila (2002), anaeleza kuwa Simiotiki ni neno la lugha ya kiyunani lenye maana ya ishara na ambalo linatumika kueleza mielekeo na makundi fulani ya kihakiki. Makundi hayo na mielekeo hiyo imezuka na mtindo wa kuzihakiki kazi za kifasihi ambapo unaangaza ishara katika kazi hizo. Kuzuka kwa nadharia hii kunahusishwa kwa kiasi kikubwa na miaka ya 1970. Wakati huo kulikuwa na mwelekeo mkubwa wa kuuasi na kuuwacha umuundo ambao ulikuwa umeutwala uhakiki wa kifasihi katika miaka ya 1960. Licha ya kuzuka kwake wakati wa simiotiki imefaidi kutokana na mawazo ya mwanaisimu wa Ki-swizi, aliyejulikana kwa jina la Ferdinand de Saussare ambaye inasemekana ndie mwanzilishi wa nadharia hii na aliungwa mkono

na mwanafalsafa wa Kimarekani aliyejulikana kama Charles-Pierce ambaye nae anahusishwa na kielelezo cha ishara kinachohusishwa na pembe tatu ambazo ni ishara, yambwa na kifasiri. Kwa mujibu wa mwanafalsafa huyu kila ishara huwa yambwa au kitendwa kinachorejelewa. Kifasiri ni kile kinachochochewa katika akili ya anayeifasiri ishara hiyo. Kimsingi tunaweza kusema hii ni nadharia inayoshughulika na ishara na uashiriaji katika kazi za kifasihi. Mwelekeo mkubwa wa nadharia hii ni kupendelea neno matini unawafanywa baadhi ya wahakiki huiita nadharia ya umatini (textuality). Baadhi ya wahakiki hupendelea neno Semiolojia baada ya Simiotiki. Suala la ishara na uashiriaji kama anavyoelezea Culler limeanza kuwa muhimu katika uhakiki wa kifasihi wa miaka ya sabiini.

Sambamba na hilo, pia mwanafalsafa huyu amekuwa muhakiki muhimu katika kuweka misingi mikuu ya nadharia hii. Mawazo yake pamoja na Julia Kristeva yameacha athari kubwa katika ukakiki wa ishara na uashiriaji katika kazi ya kifasihi. Dhana moja muhimu iliyohusishwa na Baithes ni msimbo. Kwa mujibu wa mawazo ya mtaalamu huyu, kila leksia hudhihirishwa misimbo au kaida fulani ambazo huwa muhimu katika kuifasiri.

2.6.2.1 Misimbo ya Nadharia ya Simiotiki

Barthes (1994), anaeleza kwamba kuna aina tano za misimbo inayotumika katika kazi za fasihi ambazo kwa pamoja huunda nadharia ya simiotiki. Aina hizo ni msimbo wa kimatukio, msimbo wa kihenemetiki, msimbo wa ki-seme, msimbo wa kiishara na msimbo wa kiurejelezi. Nadharia ya Simiotiki haiwezi kukamilika bila ya kurejelea mawazo ya Barthes kuhusu misimbo mitano ya usomaji ambao ni

mionganii mwa mihimili mikuu ya nadharia hii. Mtaalamu huyu anafafanua misimbo mitano kama ifuatavyo:

Msimbo wa Kimatukio: Huu unahusisha jinsi msomaji anavyouunda na kuuelewa msuko wa kazi hiyo kwa kuangalia jinsi matukio hayo yanavyofuatana kiathari au kisabasishi.

Msimbo wa Kihemenetiki: Huu nao unahusu tahaaruki na unajulikana na baadhi ya wahakiki kama msimbo wa kusimulia au kutamka hadithi. Msimbo huu unaweza kufumbatwa kwenye anuani ya kazi za kifasihi.

Msimbo wa Ki-seme: Msimbo huu unahusiana na jinsi msomaji atakavyoishia kuipata picha ya muhusika fulani wa kifasihi.

Msimbo wa Kiishara: Huu ni msimbo muhimu katika usomaji na uhakiki wa kazi za kifasihi. Msimbo huu unahusishwa na jinsi ambavyo wasomaji wanaovumbua maana ya kiishara katika kazi za kifasihi.

Msimbo wa Kiurejelezi: Msimbo huu unajengwa kutokana na viashiria vya utamaduni unaorejelewa katika kazi inayohusika. Urejeshi huu huunda uhalisi mahususi kutokana na matumizi ya vitu fulani vinavyoelewaka na wasomaji na kwanza hiyo huipa kazi fulani nguzo kitamaduni. Wamitila (2002), anasema kwamba baadhi ya wahakiki wa fasihi wanaiona nadharia ya Simiotiki ina mapungufu kutokana na kujikita zaidi kuchunguza vipengele vya lugha. Pamoja na kasoro hiyo, katika utafiti huu nadharia ya simiotiki imeonekana itamfaa mtafiti katika lengo la kwanza na la tatu ambayo yanahusiana na vipengele vya lugha.

2.7 Hitimisho

Sura hii ni sura iliyotumika kuwasilisha mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia. Mambo makuu yaliyojadiliwa katika sura hii ni pamoja na Ufafanuzi wa dhana ya methali, lugha katika methali, dhana ya dhamira, dhima za fasihi, tafiti kuhusu methali, pengo la utafiti pia lilifafanuliwa. Na mwisho nadharia teule zilifafanuliwa kwa uwazi zaidi. Nadharia hizo ni nadharia ya Simiotiki na nadharia ya Mwitiko wa msomaji.

SURA YA TATU

MBINU ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Sehemu hii inafanya uchambuzi na uwasilishaji wa mbinu mbalimbali za kukusanya data. Vipenge vilivyozingatiwa katika sehemu hii ni pamoja na mpango wa utafiti, eneo la utafiti, sampuli na mbinu za usampulishaji, data za utafiti na ukusanyaji wa data. Pia, sehemu hii imebainisha uthabiti, kuaminikakwa data na maadili ya utafiti. Vipengele hivyo vmefanyiwa uchambuzi kama ifuatavyo:

3.2 Eneo la Utafiti

Buliba, Bwachi na Matinde (2014), wanasema kwamba eneo la utafiti ni eneo la kijeografia ambalo mafiti hulifikia ili kukusanya data zake. Utafiti huu ulifanyika katika kisiwa cha Pemba ambapo data zilikusanya katika Shule ya Sekondari ya Mchangamdogo, Shule ya Sekondari Vitongoji, Shule ya Sekondari Utaani na Shule ya Sekondari ya Dokta Omar Ali Juma. Mtafiti amechaguwa maeneo haya kwa sababu ni sehemu ambayo wanapatikana wanafunzi ambao wanauelewa wa methali za jamii ya Wapemba. Hivyo mtafiti alipata data za kutosha za kujibu maswali ya utafiti huu. Mbali na wanafunzi wa shule, mtafiti pia alikusanya taarifa kutoka kwa wanajamii wa maeneo hayo ili kuchanganya taarifa za wanafunzi na watu wengine, jambo lililozifanya data zake kuaminika zaidi.

3.3 Kundi Lengwa

Kundi lengwa katika taaluma ya utafiti ni jumla ya watu wote au vitu ambavyo hutarajiwa kutafitiwa (Kothari, 2004, Bryman, 2004, Kombo na Tromp 2006). Hivyo

walengwa wa utafiti huu ni jamii ya Wapemba ambao wanaishi katika Kisiwa cha Pemba.

3.4 Sampuli na Usampulishaji

3.4.1 Sampuli

Sampuli ni kundi dogo la watu kutoka kundi kubwa linalotafitiwa ambapo kundi dogo hilo hutoa data za utafiti ambazo huwakilisha kundi lote linalotafitiwa. Hivyo basi, katika utafiti huu wateuliwa walikuwa wanafunzi 80 wa shule za sekondari. Mchanganuo wa wateuliwa unajionesha katika jadwali Na. 1 hapo chini.

Jadwali Na. 1: Sampuli ya Utafiti

Jina la Shule	Wanaume	Wanawake	Jumla
Shule ya Dkta. Omar Ali Juma Sekondari	10	10	20
Shule ya Vitongoji Sekondari	10	10	20
Shule ya Mchangamdogo Sekondari	10	10	20
Shule ya Utaani Sekondari	10	10	20
Jumla	40	40	80

Pia wanajamii kumi na wawili, watatu kutoka kila eneo la utafiti walihojiwa kuhusu utambuzi wao juu ya methali za Kipemba.

3.4.2 Usampulishaji

Usampulishaji ni kitendo cha kuchagua kikundi cha vitu au watu ili kutumika katika utafiti kama kiwakilishi cha kundi lolote linalotafitiwa (Bryman (2004). Usampulishaj ni lazima ufanyike katika mchakato wa kufanya utafiti kwa sababu si

rahisi kwa tafiti nyingi kutumia kundi lote linalotafitiwa. Hivyo, utafiti huu ulitumia mbinu ya sampuli lengwa ambayo ni utaratibu anaoufanya mtafiti kwenda moja kwa moja kwenye chanzo ambacho mtafti huamini kwamba upo uwezekano wa kupata data za kujibu maswali yake ya utafiti. Kama anavyosema Kothari (2014), usampulishaji lengwa ni kwenda moja kwa moja kwenye chanzo cha taarifa ambacho mtafiti anaamini kina uwezekano wa kumpatia data ambazo zitajibu maswali ya utafiti wake. Hivyo basi, mtafiti ameamua kutumia mbinu hii akiamini kuwa wanafaunzi wa shule alizoziteuwa walikuwa na uwezo wa kumpatia data toshelevu.

3.5 Ukusanyaji wa Data

Kwa mujibu wa Kothari (2004), mbinu za ukusanyaji wa data ni mchakato wote wa kukusanya data kutoka kwa watafitiwa tangu mwazo hadi kukamilika kwa utafiti. Katika utafiti huu data zilizokusanywa zilikuwa za msingi na data za upili. Aina hizi za data zimefanyiwa ufaanuzi kama ifuatavyo:

3.5.1 Data za Msingi

Kothari (1999), anasema kwamba data za msingi ni aina ya data zote ambazo hukusanywa kwa mara ya kwanza na mtafiti na huwa hazijatumwa na mtafiti yejote kwa lengo la utafiti kama unaofanyika. Salim (2015), anasma kwamba mara nyengine data hizi hutambulika kama data ghafi. Katika utafiti huu data za msingi zilikusanywa na mtafiti kutoka kwa wanafunzi wa shule za sekondari wa kidato cha nne hadi cha sita kama ilivyosampulishwa kwenye jedwali na.1 hapo juu.

3.5.2 Data za Upili

Hizi ni data zote ambazo mtafitin huwa anazikusanya kutoka katika tafiti zilizotangulia. Anaendelea kusema kuwa data za upili huwa na ghamara nafuu,

huokoa muda na hazitumii nguvu kubwa katika kuzikusanya (Panneerselverm, 2012). Vyanzo vya data za upili kama vinavyotajwa na Enon (1998), ni pamoja na vitabu, tasnifu, majarida, magazeti na nyaraka mbalimbali. Katika utafiti huu mtafiti ametalii machapisho kadhaa ambayo yamemuwezesha kuona pengo la utafiti huu pamoja na kupata mawazo yanayohusiana na mada ya utafiti huu.

3.6 Mbinu ya Kukusanya Data

Katika utafiti huu mtafiti alitumia mbinu ya hojaji ili kukusanya data za utafiti.

Mbinu hii imefanyiwa ufanuzi kama ifuatavyo:

3.6.1 Mbinu ya Hojaji

Kwa mujibu wa Kothari (2004), mbinu hii huhusisha uandaaji wa maswali yaliyoandikwa ambayo hutumwa kwa wateuliwa na kuwataka watafitiwa wajibu maswali hayo kwa njia ya maandishi. Maswali hayo huweza kuwa maswali fungi; ambayo humtaka mtafitiwa kuchagua jawabu ambalo tayari limeshawekwa au huweza kuwa na maswali wazi; ambayo hutoa nafasi kwa mtafitiwa kueleza majibu kutegemea na hisia au mtazamo wake. Powell na Cannaway (2004) wanatoa sababu ya kupata data kwa njia ya maswali yaliyowazi kuwa humwezesha mtu kuelewa na kufahamu mtazamo wa mtu bila kushawishi mtazamo huo kabla hawajaonesha uelewa wao kuhusu suala hilo. Hivyo, kazi ya mtafiti hapa ni kutoa muongozo ambao utawawezesha watafitiwa kujibu maswali kwa uwazi na kwa mtazamo wao kuhusu ulimwengu unaochunguzwa na kutoa mawazo yao kwa kile kinachoendelea, uzoefu wao na msingi wa utambuzi wao. Kasoro zinazoelezwa katika mbinu hii ni kwamba huwapa fursa wale wanaojua kusoma na kuandika na mara nyengine kunajitokeza kasoro ya kupotea kwa hojaji.

Ingawa mbinu hii ina kasoro za hapa na pale lakini bado mtafiti ameona kuwa mbinu hii ni moja kati ya mbinu itayomfaa katika kukusanya data. Sababu ya kutumia mbinu hii ya hojaji ni kwamba wateuliwa huwa huru kuelezea hisia, mawazo na maoni yao juu ya jambo fulani kwa uwazi zaidi. Hivyo, kwa kutumia mbinu hii mtafiti aliweza kupata data za kutosha na hatimae kujibu maswali ya utafiti huu.

3.6.2 Usaili

Usaili ni mbinu ya kukusanya data kwa njia ya mazungumzo ya ana kwa ana baina ya mtafiti na watafitiwa. Babbie (1999) na Omar (2001) wanaeleza kwamba usaili ni mbinu ya kukusanya data, kwa kuwaliza watafitiwa maswali kwa njia ya mdomo na kujibiwa kwa njia ya mdomo. Mbinu hii inaelezwa kuwa na kasoro kutokana na kutumia muda mkubwa na hata gharama na mara nyengine watafitiwa hujenga hofu. Hata hivyo mtafiti aliona kuwa mbinu hii ni ya muafaka katika utafiti huu kwani aliweza kuwapata wazee wale wanaozijua na kuzifahamu vyema methali za lahaja ya Kipemba. Vile vile mbinu hii ilikuwa ni rahisi kwa mtafiti kukusanya taarifa nyingi zilizopata fursa ya kuchambuliwa kwa kina zaidi, kwa sababu watafitiwa walipata fursa ya kuuliza maswali kuhusu methali za jamii ya Kipemba.

3.7 Usahihi, Kuaminika na Maadili ya Utafiti

3.7.1 Usahihi wa Data

Cohen na wenzake (2000), wanasema kwamba usahihi wa mbinu za kukusanya data ni utaratibu unaowezesha kupatikana kwa data sahihi na za kuaminika za utafiti. Usahihi wa data katika utafiti huu ulihakikishwa kwa kutumia mbinu ya usomaji makini na upitiaji wa nyaraka. Katika uchambuzi wa data, mkabala wa kimaelezo ndio uliotumika. Usahihi wa mbinu hizi ultokana na ukweli kuwa upungufu wa kila

mbinu moja unakamilishwa na ubora wa mbinu nyengine. Vile vile, usahihi wa mbinu na nadharia za uhakiki wa fasihi zilizotumika katika utafiti huu ziliadiliwa katika mjadala baina ya mtafiti na msimamizi wake.

3.7.2 Kuaminika kwa Data za Utafiti

Kuaminika kwa data za utafiti kunatokana na uwezo wa mbinu za utafiti kutoa matokeo yale yale ya utafiti unaporudiwa kwa kutumia mbinu zile zile (Kothari, 2008). Katika kulifafanua hili, Furlong na Lavelace, (2000), wanasema kuaminika kwa data kunajitokeza pale ambapo kunakuwa na uhusiano au ulingano katika taarifa zinazotolewa na watu wale wale kwa muda tofauti. Katia utafiti huu, kuaminika kwa data kulihakikishwa kwa kutumia ya nadharia ya Simiotiki.

3.7.3 Maadili ya Utafiti

Salim (2015), anasema kuwa maadili ya utafiti huhusishwa na mila na desturi ambayo jamii huyaamini katika eneo ambalo mtafiti analenga kuchunguza kitu au jambo fulani. Lengo la maadili katika utafiti ni kulinda mambo ya kibinaadamu yanayoaminiwa na jamii. Pia, kuhakikisha kuwa utafiti unafanyika katika muktadha unaokubalika; kwa mtu mmoja mmoja, kikundi cha watu au jamii kwa ujumla na kuhakikisha kuwa miradi ya kiutafiti inazingatia maadili, kama vile; masuala ya uongozi na athari zake, utunzaji siri na utoaji wa habari.

Miongoni mwa vitu muhimu alivyotakiwa mtafiti kuvizingatia ni maadili ya utafiti yanayohusu kupata kibali cha kufanya utafiti na kutunza siri za watafitiwa. Hivyo, katika utafiti huu, maadili ya utafiti yalizingatiwa ipasavyo kabla na baada ya kukusanya data. Kwasababu utafiti huu ulikuwa wa uwandani tulihakikisha kuwa

data zinakusanya kwa usashihi kutoka kwa watafitiwa. Pia, mtafiti alichunga maadili yanayohusiana na haki za kibinadamu. Vile vile wakati wa kuchambua na kuwasilisha data za uafiti huu mtafiti aliongozwa na nadharia ya Simiotiki kama alivyokusudia kuitumia.

3.8 Hitimisho

Sehemu hii ya tatu ya utafiti inaeleza mambo ambayo ni ya msingi sana katika kuwezesha ukusanyaji na uchambuzi wa data za utafiti. Katika sehemu hii tumeeleza mbinu zilizotumika kukusanya data na hatimae kuziwasilisha. Vipengele vilivyobainishwa katika sehemu hii ni data za upili ambazo zilitumika katika kushadadia hoja zilizotokana na data za msingi ili kuimarisha uchambuzi na matokeo ya utafiti kwa jumla.

SURA YA NNE

KUBAINISHA METHALI MAHUSUSI ZA JAMII YA KIPEMBA

4.1 Utangulizi

Kama ilivyobainishwa hapo juu lengo la kwanza la utafiti huu lilikuwa ni kubainisha methali mahususu za jamii ya Kipemba. Mtafiti alikusanya data kutoka uwandani na akapata methali kadha za jamii hiyo. Alizigawa methali zake katika makundi kutegemeana na kigezo cha maudhui zilizoshughulikiwa na methali hizo. Kwa muktadha huo makundi yake yalikuwa ni matano, yaliyohusu maudhui za kijamii, uchumi, kisiasa, kimapenzi na kiutamaduni. Orodha ya methali zinazohusu kila kundi zimeainishwa hapo chini kama ifuatavyo:-

4.2 Methali zinazoakisi Maudhui za Kijamii

Methali za aina hii ni zile ambazo zinahusu watu na harakati wazifanyazo katika jamii wanamoishi. Mfano wa methali za kundi hili ni zile zinazoendana na maudhui za kijamii ambazo ni:-

Choko tenzi waiyona mauwa

Mwenda kende

Mwenda kauyu

Kupongowa kwema, ulezi n'jakamoyo

N'ta si asali

Ntenda haneni

Vyako vyako na wenzio, vikikupata vyako pekeyo

Mambo ni matita ya kuni, kila mtu humuelemea

Nyokonyoko shiba ya kuonana

Jirani mui mlangowe uuone wazi
 Hakuna njia refu isiyofika majumbani
 Usitafunwe na uvi ukaonea tumba
 Mwanangu domo nawe waja huku hujiono
 Mgeni mja usiku hukaribishwa malalo
 Rafiki hazoi mavi ubwabwa
 Msikwenenda haono hupungua mashaka

4.2.1 Methali zinazoakisi Maudhui za Kiuchumi

Mitego mingi harabu ya nyama
 Marango n'kitu uchanga n'watu
 Toka lini punda na ujamu
 Chovyachovya humaliza buyu
 Mtoto wa kuku akikosa kazi huchakura
 Riziki na uwinda
 Kibogoyo hana Busu
 Angenda juu kipingu hafiki mbinguni

4.2.2 Methali zinazoakisi Maudhui za Kisiasa

Mja chwe huja na tena
 Mtenda wema kijuki, jazaye hutiwa moto
 Ngoma yataka Matao mcheza hawi Kiwete
 Nchama ago hanyele, hwenda akawiya papo
 Angenda juu kipungu hafiki mbinguni
 Vuli la mvumo hufunika wale kule

Chongo kwa n'yamwezi, mmanga m'macho ya kwao
 Usihadaliwe ni usiku wa kiza ukinya njiani
 Papa akipea mafuta humpa mwanawe

4.2.3 Methali zinazoakisi Maudhui za Kimapenzi

Mambo kunga, n'vungu n'keka
 Mtu huapa bamvua haapi pwa
 Usichezee kusi kwa tanga bovu
 Ukitumiavyo kipeku na kijungo utakitumia vivyo
 Miti mingine hayendwa yachana nguo mikekewa
 Jifya moja halinjiki chungu
 Ntu halindi bahari ipitayo kila chombo
 Tonga si tuwi
 Dunia kokwa ya furu

4.2.4 Methali zinazoakisi Maudhui za Kiutamaduni

Ndege wa uta hafugwa
 Msiwakwe yuna Mungu
 Nchelea ntoto wa shangazi hapati mwana
 Kimbia Ugwe Kabla hujaona Ng'ombe
 Mpanda maovu huvuna majuto
 Ndoa ni kutia nkono kizani
 Kuku wa nlimi hagwiwa

4.3 Uchambuzi wa Dhamira Vuate wa Methali za Jamii ya Kipemba

4.3.1 Utangulizi

Lengo la pili la utafiti huu ni kubainisha dhamira vuate zinazojitokeza katika methali za jamii ya Wapemba. Kulifika lengo hili mtafiti wa kazi hii alilazimika kujibu swalii lisemalo ni dhamira zipi vuate zilizojitokeza katika methali za jamii ya Wapemba? Hili lilikuwa ni swalii lililomuongoza mtafiti ili kulitimiza lengo lake la pili. Aliteuwa na kuzichambua methali zisizopungua saba zilizopo kwenye kila kundi ili kujaribu kubaini dhamira vuate iliyojitokeza. Uchambuzi wa eneo hili uliwasilishwa hapo chini kwenye kipengele (4.3.2) hadi (4.3.6).

4.3.2 Dhamira Vuate Ndani ya Methali zenyenye Maudhui ya Kijamii

Kwanza, katika kipengele hiki mtafiti alichukuwa methali isemayo kwamba, “*Choko tenzi waiyona maua*” na kuifanyia uchambuzi. Alianza kwa kuifasiri methali hii na kuiweka kwenye Kiswahili Sanifu. Katika Kiswahili Sanifu methali hii ingesemwa kuwa ‘*chooko inayotarajiwa kustawi vizuri huonekana tangu wakati wa kufumuamaua*’. Methali hii inaweza kubeba dhamira za malezi ya watoto. Kwa sababu mtoto mwenye ishara njema mara nyingi huonekana mapema kwenye uchanga wake. Hapa mtafiti wa kazi hii amenasibisha sifa bainifu za maua na sifa za mtoto mchanga kutokana na kufanana kwao kwa sifa ya umwanzo na ishara ya mafanikio. Maua ni ishara ya kuzaliwa matunda na utoto ni ishara ya muibuko wa utu uzima katika maisha ya mwanaadamu. Kwa hivyo chooko imelinganishwa na mtu mzima aliyeanzia utotoni kama lilivyofananishwa ua na mtoto mchanga. Nadharia iliyotumika kuziakisi pamoja sifa za uchanga wa ua na uchanga wa mtoto, sambamba na upevu wa mtu mzima na upevu wa chooko ni Simiotiki kupitia

Msimbo wake wa Kiseme ambao hueleza elementi nasibishi za kisemantiki ambapo hutupatia picha ya muhusika fulani wa kifasihi. Kwa muktadha huo mtafiti amefananisha ua na mtoto kwa sifa za uchanga, kama alivyoifananisha chooko na mtu mzimsa kwa sifa ya upevu. Anachokusudia kukifafanua mtafit kupitia dhamira ya malezi ni uzuri wa mtoto uchangani huakisi tabia za ukubwani, kama ilivyo uimara wa ua la chooko unavyozaa chooko njema.

Methali hii licha ya kuainisha dhamira ya malezi, pia imevuata dhamira nyengine kama vile za kiuchumi kwenye maswali ya biashara, uekezaji, uvuvi na vyanzo vyengine vya kiuchumi. Kwenye sekta ya uchumi, kupitia shughuli ya uvuvi kwa mfano, mvuvi huweza kuzibaini dalili za mafanikio bora mara tu anapoianza shughuli yake. Ikiwa mavuvi yake ya awali ni mazuri basi huweza kutabiri kiwango cha mafanikio atakayoyapata huko hatima. Utabiri wa kutokufanikiwa mwishoni pia unaweza kujitokeza kutegemeana na hali inayojitokeza mwanzo wa jambo. Methali hii mtafiti ameilinganisha na methali ya Kiswahili isemayo “Nyota njema huonekana alfajir”. Kupitia Nadharia ya Simiotiki kwenye Msimbo wake wa Kiseme ambao hueleza elementi nasibishi za kisemantiki ambapo hutupatia picha ya muhusika fulani wa kifasihi, mtafiti amenasibisha sifa za vitu viwili vilivyo ndani ya methali kisifa na hali mbili halisi zilizo katika maisha ya kila siku ya kijamii. Amenasibisha ua lenye sifa ya uchanga na umwanzo wa jambo kuwa ni ishara ya matokeo ya mwisho. Uimara wa ua la mchooko limenasibishwa na matokeo chanya na udhaifu wa ua la mti huo huo limenasibishwa na matokeo hasi iwe kwenye uvuvi, biashara, kilimo, ufugaji na shughuli nyenginezo za kiuchumi. Kwa muktadha huu methali ya Kipemba isemayo “*Choko tenzi waiyona maua*” pia imevuata dhamira za kiuchumi.

Kwa ujumla ua limetumika kitaswira kuonyesha mwanzo wa jambo na dhana “chooko tenzi” imetumika kuakisi mafanikio, kwenye shughuli yoyote inayotekelawa. Methali nyengine zenyе kuvuata dhamira sawa na zilizovuatwa na methali hii ni “kambare mkunje alimbichi”, inyoweza kutumika kuvuata dhamira ya kijamii hasa katika malezi ya watoto.

Pili, mtafiti wa kazi hii alichambua methali isemayo “*kupongowa kwema, ulezi n'jakamoyo*”. Neno kupongowa katika lahaja ya Kipemba lina maana ya kuzaa, ilhali jakamoyo lina maana ya shida na mashaka yenyе kupaparisha moyo. Kwa mantiki hii methali yetu ikiwasilishwa kwa Kiswahili Sanifu itakuwa na maana ya ‘*kuzaa watoto ni jambo zuri, ila shida kubwa hujitokeza katika wimbi la malezi*’.

Kwa uwazi kabisa methali hii imebeba dhamira ya shida katika malezi. Upembani methali hii huibuliwa na wanajamii pale mzazi wa mtoto anapopatwa na dhiki kubwa moyoni mwake kutokana na madhila yajitokezao katika mchakato mzima wa malezi ya mtoto wake. Maeleo yaliyohusu muktadha wa kimatumizi wa methali hii mtafiti ameupata kutoka kwa mtafitiwa aliyeitwa bi Mweza Mwinyi Bakari siku ya tarehe 11-04-2020 huko Jojo Mchangamdogo. Mtafiti alipomuhoji mtafitiwa wake methali hii hasa inadhamira gani? Aliambiwa kwamba, dhamira ya msingi ya methali hii ni kuonyesha jinsi malezi ya watoto yanavowatesa wazazi. Pia methali hii hutumika kutoa malalamiko juu ya mambo mbalimbali ya kijamii yanayoanzishwa na kukosa usimamizi wa dhati, mpaka yakakosa kupata ufanisi.

Mtafiti amegundua, kuitia methali hii kwamba mashaka ya ulezi imekuwa ni changamoto kubwa sana katika jamii ya Wapemba hususan kwa wakati tulionao.

Methali ya Kiswahili ambayo huvuata dhamira sawa na zile zilizovuatwa kwenye methali hii ni ile isemayo ‘*kuzaa si kazi, kazi n’kulea*’.

Tatu, mtafiti wa kazi hii alichambua methali isemayo ‘*Ntenda haneni*’, yenyé maana ya kwamba, mwenye nia ya kutenda jambo, huchagua kulitekeleza kwa vitendo kuliko kujisifia kwa maneno matupu. Watu wengi katika jamii zetu hupenda kujisifia juu ya mambo fulani wanaotarajia kuyatenda. Hata hivyo kwa bahati mbaya sana wengi hushindwa kutekeleza ahadi walizoziweka kuhusu utendaji wa mambo waliyoahidi kuyatenda. Ili kupambana na tabia hii mbovu, Waswahili hupendekeza kupitia fasihi kuachana na tabia ya kusema mambo bila ya kuyatekeleza. Wanapendekeza kwamba bora mtu atende zaidi kuliko kusemasema. Kwa muktadha huo ndiyo maana methali za Kiswahili kama “*ada ya mja kunena uungwana ni vitendo*”, “*Simba mwenda kimya ndiye mla nyama*”, na nyingine nyingi zenye uhusiano na hizi utazikuta zimejaa tele katika kumbukumbu za fasihi simulizi. Maeleo haya yanaenda sambamba na yale yaliyodiriki kusemwa na Shaaban Robert katika Adili na Nduguze (1956), alipokuwa akimsifia mfalme Rai wa nchi ya Ughaibu. Alisema kwamba ----. Kwa hivyo methali yetu ‘*Ntenda haneni*’, inasisitiza umuhimu wa kufanya mambo kwa vitendo na siyo maneno matupu yasiyo vitendo.

Kwa kutumia Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji inayotoa fursa kwa mtafiti wa kazi ya fasihi kuchambua mambo kwa uzoefu na tajiriba aliyonayo katika jamii yake, mtafiti ameshawishika kusema kwamba, tabia hii ya kusema bila kutenda imejaa tele mionganoni mwa wanajamii wa kisiwa cha Pemba. Tabia hii hudhuhiri na kukithiri zaidi mionganoni mwa wana siasa hasa siku za kampeni za kutafuta madaraka. Mtafiti kwa uzoefu wake huo, amekuwa akishuhudia ahadi kadha wa kadha zikitolewa na

wagombea wa nafasi mbalimbali. Ahadi nyingi katika hizi zinaishia hewani bila utekelezaji. Kupitia Nadhari teule, mtarifi anachukuwa nafasi hii kuishauri jamii iachane na tabia hii, kwani kwa hakika haipendezi kabisa kabisa. Methali hii kwa muktadha huu imevuata dhamira za kijamii, kisiasa na hata kiuchumi kwa kuakisi ahadi zisizotekelawa kutoka kwenye nyaja yoyote iwayo.

Nne, mtarifi wa kazi hii alichambua methali isemayo ‘*Vyako vyako na wenzio, vikikupata vyako pekeyo*’. Methali hii inaakisi tafsiri isemayo, “mtu yoyote anaeweza kuanzisha janga, vurugu au jambo bayo katika jamii kwa kiasi kikubwa anaweza kuungwa mkono na kundi ovu. Hata hivyo jambo hilo linapofurutu ada na hatimae kusababisha madhara zaidi katika jamii husika, mwanzishaji wa jambo hilo anaweza kuchukuliwa hatua zinazostahiki peke yake, bila kuhusishwa na wahusika wengine kwani ye ye ndiye chanzo cha janga hilo”. Kwa mfano kwenye jamii yetu, hasa kwenye nyanja za siasa hujitokeza fujo zinazochochewa na wanasiwa na kuungwa mkono na wafuasi mbalimbali, hasa vijana. Linapotoka la kutokea wanaofikishwa kwenye vyombo vya sharia, mara nyingi wanakuwa ni viongozi ambao ndio wapangaji wa kuu wa uchochezi uliopelekea maafa na uharibifu wa mali za umma. Mifano ipo mingi, ila tungechukuwa mfano wa matukio ya January 27, 2001 katika visiwa vya Zanzibar. Ingawa waathirika walikuwa ni wengi ila walioshitakiwa walikuwa ni viongozi waandamizi wa chama cha upinzani (CUF), kwa sababu wao ndio walioanzisha harakati za maandamano. Walioshiriki walikuwa ni wao na wenzi wao, ila waliosota rumande kwa miaka zaidi ya mitatu walikuwa ni viongozi. Kwa mtazamo wa mtarifi, kupitia Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji inayompa fursa mtarifi wa kuifasiri kazi ya fasihi kwa tajiriba aliyonayo, anaona kwamba hii ndiyo

tafsiri halisi ya methali ya Kipemba isemayo “*Vyako vyako na wenzio, vikikupata vyako pekeo.*

Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji, imempa fursa mtafiti kuweza kuishauri jamii kutovunja sharia kwa kuwatumia raia wengine hasa vijana, kwani kufanya hivyo ni kusababisha maafa yanayoweza kuepukika. Dhamira iliyovuatwa hapa ni ya kisiasa, ingawa dhamira nyengine za kijamii, kiutamaduni na hata kimapenzi zinaweza kuvuatwa na methali hii.

Tano, mtafiti wa kazi hii alichambua methali isemayo “*Mambo ni matita ya kuni, kila mtu humuelemea*”. Katika methali hii kuna vijenzi kadha vya maneno vinavyohitaji ufanuzi wa ziada ili msomaji wa Kiswahili Sanifu aweze kuielewa vyema methali hii. Kwa mfano, neno “*mambo*” linaashiria shida, kadhia nzito, mashaka na matatizo. Neno “*matita*” lina maana ya mazigo mazito yenye kuleta ugumu katika kubeba. Na hapa yamefananishwa na mazigo ya kuni. “*Kuellemewa*” iliyokusudiwa hapa ni kutatizika kwa shida zinazompata mtu. Baada ya tafsiri ya vijenzi hivi, methali hii inaweza kubeba maana isemayo matatizo na shida zinazompata mtu yoyote ni lazima zimuelemee na kumchanganya na pengine hata kumsababishia msongo wa mawazo.

Ufumbuzi huu wa vijenzi vya methali hii umetolewa kiishara kupitia Nadhari ya Simiotiki kwenye msimbo wake wa kiishara unaohusu jinsi ambavyo wasomaji wanavyovumbua maana ya kiishara katika kazi za kifasihi. Methali hii imevuata dhamira nyingi zinazojitokeza kimuktadha na hutumika kuieleza jamii kuhusu shida fulani anazokumbana nazo mtu katika kupambana na msafara mrefu wa maisha yake

au kwa jamii inayomuhusu. Methali hii inaenda sambamba na methali isemayo kwamba ‘*maisha ni safari ndefu*’. Watumiaji wa methali hii huitumia kwa kujipa faraja na kuhurumiana juu ya maswaibu na majanga mbalimbali yanayowakabili wao au jamii. Mtu hueleza maafa yanayomkabili kwa kutumia lugha ya kimethali ambayo watumiaji wa lugha ya Kiswahili huwafanya kuelewa kwa ukaribu na uwazi zaidi, kuliko kutoa maelezo fafanuzi ambayo pengine yangetumika badala ya methali. Lugha ya methali hujenga taswira inayoibua hisia za ndani za kiujumla kuliko lugha ya kawaida.

Kwa tajiriba na uzofu wa mtafiti wa kazi hii, kupitia Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji amediriki kushuhudia wanajamii kadha waliowahi kukumbwa na kadhia nzito za kimaisha, Mathalani katika jamii ya mtafiti, mtafiti alikumbana na mtu [mtafitiwa] ambaye amekabiliwa na kadhia kubwa ifuatayo: ‘Alikumbana na kufiliwa na mke wake lakini kabla siku hazijayoyoma ghafla walifariki wazazi wake wote wawili kutokana na ajali mbaya sana iliyotokea mita chache kutoka nyumbani kwao. Baada ya miezi michache iliyofuata jumba lake zuri na la kifahari liliteketea kwa moto. Jumba hili lote liliungua na hakukuwa na hata kitu kimoja kilichoweza kusalimika’. Kutokana na hali hiyo mtafiti aliweza kumsogelea na kuweza kupata taarifa zenye ufanuzi zaidi. Alipohoji ili apatiwe ufanuzi zaidi alielezwa kwa muhutasari kwa kuambiwa kuwa ewe mwanangu we ‘*Mambo ni matita ya kuni kila mmoja humuewemea*’.

Sita, mtafiti wa kazi hii alichambua methali isemayo “*Rafiki hazoi mavi, ubwabwa*” . Methali hii hutumika kuelezea mipika iliyopo kwa rafiki kumshughulikia swahiba wake. Rafiki anapaswa kumshughulikia swahiba wake kwa hali na mali, ila mambo

yanapozidi ushughulikiaji wake hulazimika kukoma, na jamaa wa damu wa swahiba anaeshughulikiwa huwajibika kukabidhiwa mtu wao ili kusudi wamshughulikie. Mtafitiwa mmoja aitwae Mwakazi Haji Makame alipotakiwa aeleze maana ya methali hii, alisema, ‘*methali hii hutumika kuonyesha mipaka ya kumshughulikia swahiba. Swahiba akizidiwa na mashaka makubwa, hulazimika kurudishwa kwa jamaa zake wa damu. Mfano mtu anayeishi ugenini, iwapo atatenda homa au kupata ugonjwa katika hatua za mwanzo, huuguzwa na kushughulikiwa na majirani na marafiki zake. Homa inapozidi jamaa zake wa karibu husakwa na kupelekewa mgonjwa wao.*

‘Mavi Ubwabwa’ limetumika kiishara kupitia Nadharia ya Simiotiki. Mavi Ubwabwa ni ibara inayoashiria hali mbaya mno anayoweza kuwa nayo mtu baada ya kukabiliwa na shida kubwa sana. Mavi ubwabwa hunasibishwa na kinyesi laini anachokunya mtu anayeharisha kutokana na maradhi thakili yanayomfika. Hali hii inapofika, rafiki humkimbia swahiba wake, na kwa yule mwenye huruma kubwa angalau humpeleka kwa ndugu na jamaa zake ili ashughulikiwe huko. Kwa tajiriba na uzofu wa mtafiti wa kazi hii, kupitia Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji amediriki kushuhudia watu wa jamii mbalimbali wakiishi nje ya jamii zao na kusuhubiana na marafiki zao huko. Wapo wengine hata kwao hukusahau. Hata hivyo watu hao wanapokuwa watu wazima au wanapopata ugonjwa, hujikuta wanarudi au wanaletwa kwao kwa ajili ya kumalizia maisha yao. Hii ndiyo maana vuate iliyojificha katika methali isemayo “*Rafiki hazoi mavi, ubwabwa*”.

Saba, mtafiti wa kazi hii alichambua methali isemayo “*Msikwenenda haono, hupungua mashaka*”. Kuna baadhi ya watu wanapenda sana upweke, hawapendi

kwenda kwenye shughuli za watu. Jambo hili huwafanya watu wa aina hii, kupungukiwa na marafiki na maswahiba wa aina nyengine kwa kuwa hawakutani na watu wa kusuhubiana nao. Pakitokea shughuli za kijamii, kama vile arusi, mazishi na harakati nyenginezo zinazohusiana na mambo hayo si aghalabu kualikwa. Kwa mantiki hii hujikuta wanaepukana na gharama za aina mbalimbali. Hawatozwi michango ya arusi, michango ya huduma za matibabu na hata mafungu ya huduma za mazishi ambayo uswahilini huitwa vichango. kwa hiyo kwa mtazamo wa juu juu hujihisi kuwa wamepungukiwa na gharama na hujihisi kuwa wao hawahusiki na jambo lolote linalohusiana na mambo hayo. Lakini ukweli ni kwamba watu hao hujitia kisumzi ng'ombe tu, kwa kujitoa mishipa ya fahamu lakini kwa kweli, bado huwa wana jukumu na dhima kubwa katika kuihudumia jamii inayowahu. Asiyekwenda haono ina maana asiyekwenda watuni hahusishwi na mambo ya watu na kuepukwa na mashaka kwa muktadha wa methali hii ni kuepukana na gharama za mambo. Hata hivyo, jambo hili huweza kumsababishia hasara kubwa muhusika, kwani wakati mwengine wanajamii wanaweza kususia mambo yake na kushindwa kutekeleza shida zinazomkabili. Pili, huu ni kinyume na utaratibu wa jamii za Uswahilini na kwa sababu hiyo anadharaulika kama anavyodharau mambo.

4.3.3 Dhamira Vuate Ndani ya Methali zenye Maudhui za Kiuchumi

Kwanza, katika kipengele hiki mtafiti alichukuwa methali isemayo kwamba, “*Mitego mingi harabu ya nyama*”. Mtafiti, munamo tarehe 23-04-2020 alimuuliza mzee mmoja mwenye tajiriba kubwa na ueledi wa hali ya juu wa fasihi ya Kiswahili, kuhusu makusudio ya methali hii. Mzee huyu ambaye anaitwa Omar Khatib Mjaka, alijibu kwamba, ‘*methali hii maana yake iko wazi na inaweza kutafsiriwa katika*

miktadha kadha wa kadha. Kiuchumi tunaweza kusema kwamba, muwekezaji mwenye vitega uchumi vingi ni rahisi zaidi kwake kupata mapato makubwa kuliko yule mwenye vitega uchumi hafifu. Mwenye madema machache kwa mfano, anatarajiwa kuvua samaki haba kuliko yule mwenye madema mengi. Madema yake mengi ni harabu ya kupata samaki wengi. Mwenye maduka mengi ya bidhaa tofauti tofauti hutarajiwa kupata faida na tija kubwa kuliko yule mwenye duka moja la bidhaa ya aina moja. Hivyo hivyo kwa wawekezaji wakubwa wenyewe viwanda. Mwenye viwanda vingi anauwezekano wa kutengeneza faida kubwa kuliko yule mwenye kiwanda kimoja au vichache. Kwa upande wa kijamii mwenye wake wengi pia ana uwezekano mkubwa wa kuwa na watoto wengi zaidi.’

Kwenye siasa pia, utakuta mwenye mtaji mkubwa wa kuchaguliwa ni yule anaeungwa mkono na watu wa sekta mbalimbali. Kwa mfano, kwa wakati mmoja anaweza kuwepo mtu mmoja anayejishughulisha na michezo, akawa anafanya kazi ofisini, anavua, analima, anakaa kwenye maskani, ni mtu wa madrasa msikitini, mwenye kushughulika na wanajamii wenzake kwenye harakati mbalimbali za kimaisha. Mtu wa aina hii, husemwa kwamba ana mitego mingi na “*mitego mingi harabu ya nyama*”. Mtu huyu hupata wapiga kura wengi kutoka kila nyanja kwa kuwa anasuhubiana na makundi mengi ya kijamii.

Nadharia ya Simiotiki kupitia msimbo wake wa kiishara inaweza kutumika kuchambua methali hii. ‘*Mitego*’ katika methali hii huashiria vyanzo tofauti vyakutafutia mapato kwenye uchumi, watoto kwenye ndoa, kura kwenye siasa na natija nyengine kwenye sekta nyengine za kimaisha. Neno ‘nyama’ limetumika kiishara kuwakilisha faida na natija zinazopatikana. Kwa muktadha huu methali isemayo

“mitego mgingi harabu ya nyama”, inaonekana kumeza maana nyingi vuate kutegemeana na sekta husika inayozungumziwa.

Pili, mtafiti alichukuwa methali ya Kipemba isemayo kwamba, “*Marango Nkitu, Uchanga N’watu*”. Katika uchambuzi wake, kwanza mtafiti alilazimika kuichambuwa methali kwa lugha ya Kiswahili Sanifu ili ieleweke vizuri. Alianza kueleza maana ya ‘*marango*’ kama inavyoolewaka kwa Wapemba wenyewe. Marango ni machagu anayokuwa nayo mtu, kwa kuteua baadhi ya vitu na kuvibea vyengine. Kwa mfano, mtu anaweza kuwa na tabia ya kupenda vyakula vya aina fulani na kutokuvipenda vyengine. Anaweza kuwa na uchaguzi wa hata aina za nguo na kuzibeza nyengine. Mtu wa aina hii hupenda kuchaguachagua vitu na kuvidharau vyengine. Lakini mtu mwenye uwezo tu, ndio mwenye fursa nzuri ya uteuzi wa vitu apendavyo na kupuuza vyengine asivyovipenda. Kwa muktadha huu ndiyo ikasemwa ‘*marango nkitu*’. ‘*Uchanga n’watu*’ ni ibara yenyé maana ya kwamba, mtu ambaye ana watu an wategemea katika kumtendea baadhi ya mambo, kila siku hujifanya mdogo anaestahiki kutendewa kila kitu kama mtoto mchanga anavyopaswa kufanyiwa na mzazi au mlezi wake.

Nadharia ya Simiotiki kupitia msimbo wake wa Ki-seme- imenasibisha marango na kipato kutohana na vitu hivi kuwa na sifa ya kusababisha. Kipato husababisha mtu kuwa na marango. Kuwa na jamaa wanaobebeba jukumu la kumtendea mtu wao mambo aliyopaswa kuyatenda mwenyewe hunasibishwa na uchanga, kwani mchanga ndie anaelazimika kutendewa. Mwenye watu wa kumtendea huitwa mchanga, ingawa pengine ana umri mkubwa. Anayejitendea mwenyewe kwa mtazamo wa

methali hii huitwa mpevu ingawa kiumri ni mdogo. Hizo ndiyo maana vuate zinazoweza kujitokeza katika methali hii.

Tatu, Methali iliyochambuliwa katika eneo hili ni ile isemayo “*Toka lini punda na ujamu*”. Punda ni mnyama mashuhuri katika baadhi ya sehemu kisiwani Pemba. Matumizi makuu ya mnyama huyu ni kubebea mizigo. Si aghalabu mnyama huyu kutiwa hatamu puan au kwenye pembe kama vile afanywavyo ng’ombe. Kumtia Punda ujamau hatamu ni kufanya jambo lililo kinyume na mazowea au uhalisia. Kufanya hivyo ni kuwashangaza watu na kumtia dhiki Punda. Methali hii hutumika kuelezea bezo na dharau dhidi ya mtu anaetarajia kupata kitu kinyume na hadhi yake. Kwa mfano, iwapo kuna mtu maskini aliyeokuwa na mwelekeo wa kufuzu kibiashara na mara moja akaharibikiwa, kukosa bahati kwake huelezea kwa kuuliza swal, ‘*tangu lini punda na ujamu*’?

‘*Punda na ujamu*’ni maneno mawili yaliyotumika kiishara kwa kutumia Nadharia ya Simiotiki kupitia msimbo wake wa Kiseme unahusiana na jinsi msomaji atakavyoishia kuipata picha ya muhusika fulani wa kifasihi. Kupitia Nadharia hii punda amenasibishwa na mtu asiyebahati au masikini asiyezowea kupata na ujamu umenasibishwa na bahati njema aliyonayo mtu mwenye utajiri au mazowea ya kupata. Kwa hivyo masikini anapoharibikiwa na jambo ambalo awali lilionyesha sura

ya mafanikio, ubaya wa bahati yake huelezwa na jamii iliyomzunguka kwa kusemwa toka lini ‘*punda na ujamu*’. Maelezo ya methali hii hutumika kama aina fulani ya shere au kebehi dhidi ya muhusika (masikini) aliyeharibikiwa.

Nne, mtafiti wa kazi hii amechambua methali isemayo “*Angenda juu kipingu hafiki mbinguni*”. Kabla ya kuichambua methali hii, mtafiti alilazimika kuchambua vijenzi vyatya methali wenyewe. Neno ‘*angenda*’ limefupisha ibara iliyojengwa na maneno mawili; ‘*ingawa na ataenda*’. ‘*Kipingu*’ni aina ya ndege jamii ya kozi/mwewe anayepaa na kuelekea angani. Ndege huyu fahari yake kubwa ni kujipeleka mbali inavyowezekana katika anga za juu. Ndege huyu ametajwa katika methali hii kuwakilisha juhudi za hali ya juu ya kupigania jambo alitakalo mtu. Vyovyote viwavyo kufikia lengo lililokusudiwa si jambo rahisi kwa wengi wapiganiao jambo. Hata hivyo viwango vyatya mafanikio hutofautiana kati ya mtu mmoja na mwengine.

‘*Kipingu*’ ametumika kumuwakilisha yule anaejitahidi sana katika kukimbilia kiwango fulani cha mafanikio. Hii imekuja kupitia Nadharia ya Simiotiki kwenye msimbo wake wa Ki-seme. Kupitia msimbo huu pamefanyika unasibishi baina ya kipingu na yule anaejitahidi. Watu wa aina hii wamenasibishwa na kipingu kwa kuwa kipingu huweza kufanya jitihada kubwa zaidi na kwa kadiri ya uwezo wake ili kusudi aweze kufikia kikomo chake labda kwa fikra zake aweze kufika mbinguni, ambako ndiko kwenye kikomo chake. Vivyo hivyo binaadamu unakuwa ni mwenye kuonyesha jitihada kubwa katika kujikwamua na hali ngumu ya maisha. Huweza kufanya juhudi kubwa iwezekanavyo ili aweze kuwa na maisha mazuri zaidi, lakini mafanikio vyovyote yawavyo huwa hayamtoshelezi na kwa hivyo huyahesabu kuwa yako chini ya kiwango akitakacho. Neno mbinguni limewakilisha ukomo uliokusudiwa ambao unakuwa ni mgumu kufikiwa na yule anaejitahidi kuukimbilia.

Tukimmithilisha Raisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuwa ni kipingu kwa azima yake ya kukimbilia urchumi wa kati na kujenga Tanzania ya viwanda ifikapo

2025, anaonekana kuwa na mafanikio fulani, lakini kila ajisogezavyo usoni bado kwanza hujiona hajatosheka na pili kuna changamoto nyingi bado zinaingilia kati, hivyo kufanya azima yake kudorora kidogo au kukwama katika baadhi ya maeneo. Kwa muktadha huu kwa lugha ya kawaida husemwa ingawa juhudi inafanyika na mafanikio yanapatikana ila kufikiwa kwa malengo kunakabiliwa na changamoto kadha. Maelezo haya ndiyo yanayoenda sambamba na methali isemayo “*Angenda juu kipingu hafiki mbinguni.*”

Tano, mtafiti wa kazi hii alichambua methali isemayo kwamba, “*Mtoto wa kuku akikosa kazi huchakura*”. Mtoto wa kuku kwa muktadha wa methali hii ni mtarazaki anayejitafutia njia za kujikimu. Huyu ni mtu wa kipato cha chini kabisa anayepata riziki yake kwa njia ya kuungaunga. Hana shughuli maalum ya kupata kipato cha kuendesha maisha yake. Kupitia nadhari ya Simiotiki kwenye msimbo wake wa kiishara, hapa pametumika ishara ya mtoto wa kuku wa kienyeji kumfananisha na mjasiri amali asiyé na shughuli maalum, kwa sababu kuku wa kienyeji hana uhakika wa kipato chake, wapi kitatoka na kiasi gani atafanikiwa kujaza bofu lake. Ishara ya mtoto wa kuku imetumika kumuwalilisha masikini, kwa kuwa ni kawaida ya watu waliowengi wenye ajira zisizorasmi kujihusisha na kazi mbalimbali, almuradi wapate riziki itakayowawezesha mkono kwenda kinywani. Kuchakura kwa muktadha uliokusudiwa ni kuhangaika huku na kule kutafuta kazi nyengine baada ya kazi ya awali kumalizika, kwa sababu ya kutokuwepo kazi maalum ya kufanya. Mjasiri amali wa aina hii hawezi kukaa bila ya kazi, lazima kazi aitafute ili kupata njia za kujikimu na hii ndiyo maana ya “*Mtoto wa kuku akikosa kazi huchakura*”.

Sita, mtafiti aliangazia methali isemayo “*Riziki na Uwinda*”. Katika methali hii mtafiti alieleza maana ya vijenzi vya methali kwa kuiangalia kamusi la (BAKIZA) (2010), ambalo limefasiri kuwa ‘*riziki*’ ni kipato fulani anachokipata mtu katika maisha yake au juu ya shughuli fulani anayoifanya. Kwa itikadi za mafunzo ya dini ya Kiisilamu na pengine hata dini nyengine, kila mja amewekekewa riziki yake na mipango ya riziki imepangwa na Mungu tangu azali kabla binaadamu hajaja ulimwenguni bado. Kwa msingi huu riziki ya mtu haiongezeki wala haipungui juu ya kiwango mtu alichopangiwa na mola wake. Pamoja na ukweli huu hata hivyo binaadamu anatakiwa afanye kazi kwa bidii kubwa ili kuisaka na kuitafuta riziki hiyo. Anatakiwa aiwinde riziki yake kama mnyama anavyowinda malisho na maji porini kwa lengo la kujikimu kwa shinda ya njaa na kiu. Neno uwinda lililotumika katika methali hii lina maana ya usakaji nautafutaji wa kitu kwa bidii kubwa. Kwa mantiki hii kitakiwacho kwa binaadamu ni kujitahidi sana kufanya kazi ili kujitafutia mahitaji ya kujikimu. Hapaswi kukaa tu na kusema mimi nina riziki zangu sina haja ya kuhangaika. Ni kweli riziki zimepangwa na Mungu, lakini Mungu huyuhuyu ndie aliyehimiza umuhimu wa kufanya kazi na kujituma. Kwa hivyo msingi wa kiimani juu ya riziki za mja haupingani na ulazima wa kufanya kazi. Mama mmoja wa Makamo alisema neno ‘*uwinda*’ halitokani na dhana ya kusaka wanyama, lakini linatokana na kivazi chenye muundo wa chupi itengenewayo kwa shuka inayokunjwa itumiwayo na wapanda minazi au mikarafuu mikubwa. Kwa hivyo, kwa mujibu wa mama huyu mtu anatakiwa lazima apige winda ili afanye kazi kwa lengo la kujipatia riziki yake. Kwa muktadha huu “*riziki na uwinda*”ina maana ya kwamba, ‘*riziki*’ ya mtu ipo, lakini na haja ya kujitahidi katika kuitafuta ni jambo la lazima. Hii hasa ndiyo maana ya “*riziki na uwinda*”.

Saba, mtafiti wa kazi hii alifanya ufanuzi wa methali isemayo kuwa, ‘*Kibogoyo hana Busu*’. Kibogoyo kw mujibu wa BAKIZA (2010) ni mtu aliyeng’oka meno mengi na kubokoka mdomo, ilhali busu ni mguso maalumu wa midomo juu ya shavu au mkono wa mtu kuashiria furaha, heshima au mapenzi. Mtu asiyehi meno hawezikabis kupiga busu likaelekeaa kuleta ufanisi. Hii ni kwa sababu mpiga busu hutakiwa aufume muundo wa mdomo kwa kuuvuta mbele, jambo ambalo linategemea sana kuwemo kwa meno kwenye kinywa. Ukosefu wa meno husababisha uzito wa kuurekesisha mdomo namna apendavyo mpiga busu. Hii ni maana ya kawaida sana ilinayotokana na vijenzi vya kawaida vya methali hii. Lakini kimuktadha, methali hii imebeba maana vuate kadha zilizojificha ndani yake. Maana hizi mara nyingi hujitokeza kutokana na muktadha wa kimatumizi.

Nadharia ya Simiotiki kupitia msimbo wake wa Kiishara unaohusiana na jinsi msomaji atakavyoishia kuipata picha ya muhusika fulani wa kifasihi. Kupitia nadharia hii, neno kibogoyo limetumika kiishara kuwakilisha mtu asiyehi rasilimali muhimu za kutekeleza jambo kwa kiwango maridhawa kitakiwacho. Busu ni ufanisi wa jambo utakiwao kufikiwa baada ya jamobo fulani kufikiwa. Kwa hivyo methali isemayo ‘kibogoyo hana busu’ imevuata maana ya kimuktadha inayoeza kuelezwakwamba ‘mtu yoyote asiyerasilimali, ifaayo kutenda jambo lake kwa ufanisi hawezikabisa kutenda jambo hilo likaelekeaa. Maana kama hizi za kimuktadha katika methali zilielezwa vizuri na Sheha (2019), ambaye anasema maana ya methali ni za aina mbili; maana ya wazi inayotokana na vijenzi vya methali na maana ya kimuktadha ambavyo ndio inayokusudiwa kuwasilishwa kifasihi.

Bibi Mboja Ali Hamad wa Vitongoji mwenye umri wa miaka sabiini na minane (78) alihojiwa kuhusu makusudio ya methali hii ya Kipemba. Mahojiano hayo yalifanyika siku ya tarehe 14-05-2020. Kwenye jibu lake -alisema “*metha hii hutumiwa kuonyesha uwezo mdogo aliokuwa nao mtu katika kufanya jambo. Mfano mtu anaweza kuulizwa, wafanya harusi hata karamu inkushinda. Muulizwa hujibu, ndugu yangu we, kibogoyo hana busu.*” Hii inaonyesha kwamba aliyeulizwa juu ya kwa nini hakufanya karamu, huwa anaashiria uwezo hafifu alionao juu ya utekelezaji wa jambo fulani.

4.3.4 Dhamira Vuate Ndani ya Methali zenyenye Maudhui ya Kisiasa

Kwanza, katika kipengele hiki mtafiti alichukuwa methali isemayo kwamba, “*Mtenda wema kijuki, jazaye hutiwa moto*”. Nyuki ni mdudu jamii ya dunduvile. Ni mdudu mwenye hadhi na thamani kubwa katika jamii. Mara nyingi huzalisha zao liitwalo asali. Kwa miaka mingi nyuki amekuwa akiishi kama mdudu msitu ambae zao lake la asali huvunwa kwa kumchoma moto yeye mwenyewe kwanza. Ille kumchoma moto hufanywa na wavunaji wa asali ili kujikinga na vishindo vyake vya kuwanata, hasa kwa kuwa mdudu wenyewe anasababisha maumivu makali anapomnata mtu. Hata hivyo, hivi sasa njia za kitaalamu hutumika kuwafuga wadudu hawa na kwa hivyo asali yao sasa huvunwa pasina kuwachoma moto.

Tukichukulia huo muktadha wa kizamani, nyuki pamoja na wema wake wa kutengeneza asali, alikuwa akijikuta anachomwa moto ili watu wajipatie asali aliyoitengeneza kwa jasho lake. Haya kwa hakika yalikuwa ndio malipo yake. Kwa msingi huu ndio methali isemayo “*mtenda wema kijuki, jazaye hutiwa moto*”. Hii ni tafsiri ya methali hii kwa kuangazia mtizamo wa kawaida.

Tunapokuja kwenye mtazamo wa kinadhari, tunagundua kwamba, msimbo wa kiseme wa Nadharia ya Simiotiki umetumika kunasibisha malipo mabaya alipwayo mfanya wema yoyote katika jamii ya watu. Kwa lugha nyengine tunaweza kusema kwamba, mtenda wema anayelipwa mabaya hufananishwa na nyuki atengenezae bidhaa bora, muhimu na adimu na hatimae akachomwa moto wakati wa uvunaji wa bidhaa hiyo. Jamii zetu mara kadha hushuhudia maovu makubwa walipwayo watenda wema ambao wema wao ulifika kuzikomboa jamii hizo. Kwa mfano, muheshimiwa Abeid Amani Karume; jamadari wa mapinduzi ya Zanzibar, aliifanyia mengi mema jamii ya Zanzibar ila jaza ya mema yake ilikuwa ni kuuliwa na baadhi ya wapinga maendeleo wa jamii hiyo ya Zanzibar.

Baadhi ya wale walioguswa na kifo cha Karume walikuwa wakitumia sana methali hii kumsikitikia na kuonyesha huzini juu yake. Mbali ya wema wake, lakini bado jaza yake ilikuwa ni kuuliwa kwa kumiminiwa risasi zaidi ya nane. Wema wake haukuzingatiwa na wapinga maendeleo hawa; kwa kuwa “***Mtenda wema kijuki, jazaye hutiwa moto***”.

Katika nyanja za kimataifa kwa mfano, kiongozi wa Libya Muamari Gadafi alikuwa mwema sana kwa watu wake. Alizimarisha sana huduma na ustawi wa raia zake. Watu walisoma bure huko na walitibiwa bila kulipia huduma za afya. Inasemekana kuwa waliokosa ajira walikuwa wakilipwa fedha za kujikinu. Kwa ujumla kiongozi huyu alikuwa muadilifu na mwema kwa watu wa Libya. Chokochoko zilianza na hatimae vita vya wenyewe kwa wenyewe ikazuka. Nguvu za kijeshi kutoka ndani na nje ziliiteteresa nchi ya Libya na hatimae Gadafi akauliwa, yalimfika yale ya ‘mfanya wema kijuki’. Jaza yake ilikuwa ni kuuliwa kinyama na kundi la raia wa

Walibya waliopingana na mtazamo wake. Ama kwa hakika yaliyomkuta Gadafi yanaakisi ukweli wa methali isemayo “***Mtenda wema kijuki, jazaye hutiwa moto***”.

Pili, mtafiti alichambua methali isemayo “*ngoma yataka matao mcheza hawi kiwete*”. Alianza kufasili neno ngoma ambapo alisema, ngoma ni mdundo wa ala maalum ya muziki unaopigwa kwa mfumo fulani kutegemeana na aina ya ngoma iliyokusudiwa, (BAKIZA 2010). Ngoma hupigwa katika jamii mbalimbali kwa malengo yanayotofautiana. Ngoma zipo za aina nyingi, na majina yake hutofautiana kati ya ngoma moja na ngoma nyengine kwa kigezo cha tofauti za mipigo, namna ya uchezaji na chanzo au historia ya ngoma wenyewe. Kikawaida kila ngoma ina namna ya uchezaji wake na mbinu zake. Baadhi ya ngoma inahitaji ukamilifu wa viungo, mwenye kasoro ya viungo hawezi kuicheza. Ina mbinu zitakiwazo kukamilika kwa kuwa na ukamilifu wa viungo. Mlemavu wa viungo kama miguu, mikono na pengine hata nyonga, mbwembwe zitakiwazo hawezi kuzifikia. Kwa muktadha huu tunaweza kusema kwamba, “*Ngoma yataka matao mcheza hawi kiwete*”. Muktadha uliobainishwa hapa ni wa kikawaida na uchambuzi wake umezingatia lugha iliyotokana na vijenzi vya methali hii.

Lakini tukitumia uchambuzi wa ndani unaotumia misingi ya nadharia, tutagundua kwamba, neno ‘*ngoma*’ limetumika kama kiwakilishi kinachoashiria jambo kubwa na gumu linalomkabili mtu au jamii inayomzunguuka. Ni jambo linalohitaji mtu mwenye mbinu na ufundi wa hali ya juu ili aweze kulitekeleza. Anaetaka kulitekeleza bila ya mbinu na ufundi utakiwao hatofikia malengo yatarajiwayo. Neno ‘*matao*’ linawakilishi ufundi na mbinu zifaazo katika utekelezaji wa jambo

lililoashiriwa hapo juu. Mtu yoyote asiyeweza kulitekeleza huambiwa kwamba ni kiwete.

Nadharia ya Simiotiki kupertia msimbo wake kiishara unahusishwa na jinsi ambavyo wasomaji wanavyovumbua maana ya kiishara katika kazi za kifasihi. Kupertia nadharia hii neno ‘*ngoma*’ limetumika kuashiria ugumu wa shughuli kubwa iliyokusudiwa kutendwa na mtu au jamii ya watu fulani. Neno ‘*matao*’ limewekwa katika methali hii kuashiria mbinu na ufundu mkubwa alionao mtu anayetarajiwa kulikabili jambo gumu lililooneshwa kiishara kwa kutumia neno ‘*ngoma*’. Neno ‘*kiwete*’ kwenye methali hii limetumika kuashiria mtu asiye uwezo ambaye anataka kushiriki katika utendaji wa jambo, hali ya kuwa hana mbinu wala ujuzi wa kukabiliana na jambo wenyewe.

Muktadha wa methali hii unatuonyesha kwamba siyo vizuri hata kidogo kwa mwanajamii kushiriki kazi yoyote asiyokuwa na ujuzi nayo. Kufanya hivyo ni kosa na kutakoseha ufanisi wa kile kinachotendwa. Mtu asiyejua elimu ya tiba hawezi kutibu mgonjwa. Kumtibu mgonjwa kutaleta madhara kwa sababu mtu huyu anacheza ‘*ngoma*’ si yake, anaingia kwenye ‘*ngoma*’ asiyokuwa na ‘*matao*’ nayo. Lazima anayetibu ajue kwamba, ‘*ngoma yataka matao mcheza hawi kiwete*’. Mama mmoja wa makamu aliyeitwa Hidaya Khatib Mjaka alipokuwa akihojiwa siku ya tarehe 21-05-2020, “*makusudio ya methali hii ni kuwafahamisha watu, kwamba kila jambo lina kunga na siri zake. Lina mbinu na ufundu wa kulikabili. Mtu hawezi kwea mnazi kama hata mbingu hawezi kuiweka sawa miguuni. Nadhodha wa chombo baharini nae pia hutakiwa awe na ubingwa na ujuzi wa kukipeleka chombo kwa kutumia alama za kimaumbile, mabadiliko ya upopo na mienendo ya mkondo wa*

maji baharini”. Anayetaka kufanya jambo bila kulisomea ajue anakusudia kuingia kwenye ‘*ngoma*’ ambayo siyake. Yeye ni ‘*kiwete*’ ambaye bila shaka hatoweza kucheza vyema kwa kukosa ‘*matao*’ ya ‘*ngoma*’ hiyo. Kwani “*ngoma yataka matao mcheza hawi kiwete*”.

Mtafiti kwa hivyo, anaona kwamba methali hii inabeba maana nyingi vuate kutegemeana na muktadha wa matokeo yalivyojitokeza. Kwa mfano, asiyejua mbinu za soka hawezi kucheza soka vizuri, kwa sababu siyo fani aijuwayo. Asiyesomea ualimu hawezi kufundisha vizuri kwa sababu ualimu si fani yake. Asiyejua kutweka chombo baharini, hawezi kuwa nahodha mzuri, kwa sababu hana mbinu za kusafirisha abiria kupitia njia hii. Hii ni kwa sababu “*ngoma yataka matao mcheza hawi kiwete*.”

Lakini pia katika medani ya siasa, iwapo mtu hajui chochote kuhusiana na mambo ya siasa, itakuwa ugumu kwake, kuweza kugombania au kuteuliwa kushika nafasi yoyote inayohusiana na tasnia hii, kwa sababu siasa si fani yake. Kwa muktadha huu tunashadidia hoja yetu ya kuwa ‘*ngoma yataka matao mcheza hawi kiwete*.’

Tatu, mtafiti wa kazi hii alifanya uchambuzi wa methali ya Kipemba isemayo “*mchama ago hanyele hwenda akawia papo*”. Moja miiongoni mwa maana ya neno ‘*chama*’ katika Kipemba ni ‘*hama*’. Kumchama mtu, maana yake ni kumuhamama. Kuchama mahali, maana yake ni kuikimbia sehemu hiyo. ‘*Ago*’ kwa mujibu wa kamusi ya BAKIZA (2010) ni ‘*mahali wanapofikia wavuvi na kendeleza shughili hiyo*’. Hiyo ni kambi ya uvuvi ambayo hutumika kama mahali pa kuishi wavuvi hao kwa muda wote wa miezi kadha ambapo uvuvi unaendelea. Mahali hapa panakuwa

ni mbali na makaazi ya asili ya wavuvi hawa. Kwengineko jina ‘*dago*’ hutumika badala ya ‘*ago*’na wengine hutumia neno ‘*kigono*’ kuwasilisha dhana hii. Kwa maana ya dhahiri inayoibuka kutokana na vijenzi vilivyojenga methali hii “*mchama ago hanyele*” ni kwamba, mvuvi aliyeamua kuondoka kambini kwa muda au kwa lengo la kutorejea tena sehemu hii hatakiwa kabisa kupaharibu mahali hapo, kwani inaweza kutokea akarejea akapahitaji mahali hapo. Kama amepachafua kwa kuweka kinyesi au matakataka mengine, itamlazimu asafishe na apatengeneze upya, jambo ambalo litampa usumbufu mkubwa.

Katika muktadha wa kimatumizi methali hii huvuata maana kwa mujibu wa mazingira yaliyojitokeza. Kwa mfano, mtu anaeamua kumuacha mke kwa mujibu wa mitazamo na sharia za Kiislamu, hutakiwa amwache kwa wema ikilazimika au aendelee kukaa naye kwa wema. Iwapo atamuwacha kwa matusi na kumfedhehesha itakuwa ni vigumu kumrejea na kuishi nae kwa heshima. Kwa muktadha huu ndio mume hufunzwa na kuusiwa na sheikhe muozeshaji kwamba iwapo atalazimika kumuwacha mke huyo basi amwache kwa wema; Quran (2:231). Mafunzo haya yanampa fursa muoaji kurejea tena iwapo atataka kufanya hivyo baada ya kuwachana naye. Kwa upande wa siasa kwa mfano, mtafit wa kazi hii kutokana na uzoefu wake na tajiriba ya maisha aliyonayo kupitia nadharia ya mwitiko wa msoaji ameshuhudia kwa awamu mbalimbali kuwepo kwa wanasiasa wa vyama mbalimbali mionganoni mwa vyama vilivyopo nchini kuvihama na kuvikejeli vyama vyao vy aasili. Kimsingi mwanasiasa hatakiwi kufanya manyago katika chama chake, badala yake anahotakiwa ni kukienzi na kukitunza chama hicho. Lakini pale ambapo atateleza au kukikosea nidhamu chama chake cha awali, hapaswi kukikashifu wala

kukikejeli huku akifikiria kwamba hatorejea tena katika chama hicho, katika kipindi ambacho anaenda kuhamia kwenye chama kipywa. Kwa mfano, utakuta kwenye harakati za hamahama ya vyama kwa wanasiasa, wapo baadhi ya viongozi ambao huhama kutoka chama kimoja kwenda chama kingine huku wakitoa matusi ya kashfa na kuvilaani vikali sana vyama vyao vyaa awali, lakini husahau kuwa “*mchama ago hanyele hwenda akawia papo*”.

Neno ‘ago’ limetumika kiishara kupitia msimbo huu kisimiotiki, kuonyesha mahali ambapo mtu anapatumia kuendesha shughuli zake za kimaisha. Kwa mfano mvuvi huitumia kambi kama ago lake, mwalimu naye sehemu ya kazi au shule aliyopangiwa kufundisha ndilo ago lake, vikosi vyaa ulinzi na usalama katika naeneo yao ya kufanya kazi, hilo hutambulika ka-a ago lao, matabibu na wauguzi hupatumia wanapofanya kazi kama ‘ago’ lao. Kwa ujumla mtu yoyote hatakiwi kuliwacha eneo lake la kazi kwa jeuri, dharau na kejeli kwa kufikiria kuwa halite-faa tena katika maisha yake.

Nne, mtafiti wa kazi hii amechambua methali isemayo “*Vuli la mvumo hufunika wale kule*”. Kwa mujibu wa BAKIZA (2010), mvumo ni mti mrefu wenye kigogo kinene na kivimba katikati bila ya matawi wenye majani yanayofanana na muwaa unaozaa matunda kama nazi. Kwa kuwa mti huu ni mrefu basi jivuli lake linakuwa mbali na pale lilipo shina hasa nyakati za asubuhi mapema na jioni sana. Wakati wa asubuhi jivuli linakuwa mbali upande wa magharibi na wakati wa jioni vuli lake linakuwa mbali upande wa mashariki. Umbali wa jivuli lake unatokana na yale maumbile yake ya kuwa na majani mwishoni tu na ile hali yake ya kukosa matawi. Nadharia ya Simiotiki kupitia msimbo wake wa kiseme inaweza kutumika hapa kunasibisha mtu

anaewakimbia jamaa zake wa karibu na kwenda kuwanufaisha wengine mbali na vuli la mvumo. Daima mvumo huvisitiri zaidi kwa kivuli chake vile vilivyo mbali yake upande wa mashariki au magharibi kutegemeana na wakati aidha wa asubuhi au wa jioni.

Methali hii ni nzuri sana kuitumia kwa wanasiasa wanaoomba kura kwenye majimbo ya uchaguzi, ambao huhama na kwenda kuishi miji mingine mara tu baada ya kuchaguliwa. Huwakimbia kabisa wapiga kura wao na faida na manufaa ya vyeo walivyokabidhiwa huwafikia wengine, wanaoishi pamoja nae kule walikokimbilia. Shina na msingi wa kufaulu kwake uko kwengine, lakini wafaidikao pia ni wengine wasiohusika na chanzo na msingi wa mafanikio hayo.

Methali hii pia inaweza kutumika kwa vijana wasomeshwao vijijini kwao na baadae wakahamia mijini kuendeleza maisha pale wapatapo kazi za kujikimu. ‘*Shinani kwa mvumo*’ kwa muktadha wa methali yetu hii ni kule kijijini ambako vijana hawa wamesomeshwa na kule ambako ‘*jivuli hufunika*’ni kule mbali na kwao kwa asili ambako huishi huko kwa kuendeleza na kutumbua maisha. Kisimiotiki kupitia msimbo wake wa Kiseme dhana ‘*shina la mvumo*’ imetumika kunasibisha makaazi ya asili ya mtu na uasisi wa mafanikio ya mtu huyo. Jivuli imenasibishwa na natija na faida anayoipata mtu baada ya kujifunza au kujihusisha na shughuli yoyote inayompa kipato. Kwa hivyo methali hii haitumiki kwa yule anaepatamaslahi na kuyatumia kwa kuwasaidia wale wale waliopo kwenye eneo lake la asili.

Katika uzoefu wake na tajiriba aliyonao mtafiti kupitia Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ameshawishika kusea kwamba, kuna baadhi ya vijana wa Kizanzibari

ambao walipata elimu na ujuzi wao mkubwa katika visiwa vyao vya Zanzibar lakini taaluma yao hiyo wanaitumia katika nchi wanazoishi sasa za ughaibuni au kwengineko na hatimae huonekana katika mataifa hayo wanayoishi yamepiga hatua kubwa kimaendeleo. Vijana hawa huwa wanatoa michango mikubwa ya maendeleo ya mataifa hayo waliyohamia baada ya kupata elimu zao hapa Zanzibar. Vijana hawa wameenea maeneo mbalimbali ya ulimwengu wakitoa michango yao kupitia vipaji tofauti walivyonyavyo. Wapo wanaotumia elimu zao kufundisha vyuo vikuu vya nje, wapo wahandisi wajenzi wa miundo mbinu mbalimbali na watumishi wengi wengineo.

Tano, mtafiti wa kazi hii, ameamua kuchambua methali isemayo ‘*Chongo kwa n'yamwezi mmanga m'macho ya kwao*’. Mnyamwezi ni mtu wa kabila maalumu mionganoni mwa makabila ya Kanda ya Ziwa huko Tanzania Bara. Kabila hili lina uhusiano wa karibu sana na kabila la Kisukuma. Watu wa kabila hili hupatikana kwa wingi katika mikoa ya Tabora, Shinyanga, Simiyu na Mwanza. Kwa mtazamo wa watu wa visiwani watu wote kutoka Tanzania Bara ni Wanyamwezi. Mnyamwezi katika jamii ya Zanzibar, alihesabiwa kama mtu duni asiyehadhi. Kazi yake kubwa ilikuwa ni kupewa kazi za kilimo na kubeba mizigo mizito ya matajiri waliokuwepo katika jamii wakati huo. Matajiri wakubwa wakati huo walikuwa Waarabu na Wahindi. Mara nyengine Wanyamwezi walipewa shughuli za kulinda na kusimamia mashamba ya matajiri hao.

‘*Mmanga*’ni mtu wa kabila moja wapo mionganoni mwa makabila ya Kiarabu. Watu wanaoitwa Wamanga ni Waarabu wenye asili ya Maskati Oman. Zamani kabla ya

Mapinduzi ya Zanzibar ‘*Mmanga*’ alionekana na hadhi kubwa visiwani, hasa Pemba ambapo watu hawa walikaribishwa na kupewa hadhi kubwa katika jamii.

Waarabu kwa wakati huo walipewa ubwana na makosa yao kwa jamii yalikuwa hayahesabiwi kuwa ni makosa. Kwa muktadha huu, ‘*Mnyamwezi*’ aliadhibiwa hata kwa kosa dogo na ‘*Mmanga*’ hakukosea kwa taa wa kijaii hata kaa katenda jinai kubwa kama vile la kuuwa lakini kwa jamii hiyo hakuweza kughadhibiwa kutokana na kosa lake hilo.

Methali hii hutumika kuonya na kutoa tahadhari juu ya tabia ya ubaguzi na upendeleo unaofanywa na baadhi ya wasimamizi wa maswali ya sharia. Aliyeniyimwa haki katika muktadha huu hunasibishwa na *Mnyamwezi* na yule aliyependelewa hunasibishwa na *Mmanga*. Kosa la aina moja likibeba adhabu kwa mshitakiwa mmoja na samaha kwa mshitakiwa mwengine, ndiyo husemwa ‘*Chongo kwa n’yamwezi mmanga m’macho ya kwao*’, ikiwa na maana kuna uonevu na ukandamizaji wa mtu mmoja na upendeleo kwa mwengine.

Kinadharia mtafiti wa kazi hii ametumia nadharia ya Simiotiki kupitia msimbo wake wa Kiseme kuzinasibisha pamoja sifa ya mwenye hadhi ya chini na sifa ya *Mnyamwezi* kama alivyokuwa akihesabiwa wakati wa ukoloni. Kama tulivyotangulia kusema mtu wa kabilia hili alidharaulika sana kipindi hicho. Mwenye hadhi ya kuchukuliwa kwamba tendo lake ovu siyo kosa alinasibishwa na *Mmanga* kama ilivyoaminiwa na jamii wakati wa ukoloni. Mwenye kuadhibiwa kwa kosa lake au pengine kuonewa kwa mujibu wa methali hii ni *Mnyamwezi* na anaesamehewa kosa au pengine kupendelewa kwa muktadha huu ni *Mmanga*.

Mtafiti kwa uzoefu alionao na tajiriba ya maisha aliyoipata kwenye jamii yake kupidia Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ameibuka na fikra isemayo kwamba, methali hii imewapa hadhi na nafasi kubwa watu wa kabile la Waarabu na kuwadhalilisha Wanyamwezi na makabila mengine ya watu weusi jambo ambalo linapelekea kuzuka kwa matabaka na ubaguzi wa rangi katika jamii jambo ambalo linapigwa vita vikali sana na jumuia zote Uliwenguni kama vile Umoja wa mataifa, Umoja wa nchi za Ulaya, Jumuia ya madola, Umoja wa Afrika, Jumuia ya Afrika Mashariki pamoja na taasisi za serikali na za watu binafsi.

Sita, mtafiti wa kazi hii ameamua kuchambua methali isemayo '*Usihadaliwe ni usiku wa kiza ukinya njiani*'. Kupitia Nadhari ya Simiotiki kwenye msimbo wake wa kiishara mtafiti amepata fursa ya kuchambua fumbizi zilizomo kwenye methali husika. Neno '*usiku wa kiza*' linaashiria fursa za kile kinachodaiwa kuwa ni demokrasia ya kutoa maoni aliyonayo mtu wakati wa harakati za kisiasa. '*Kunywa njiani*' inaashiria utowaji wa maneno machafu dhidi ya serikali au uchochezi unaoweza kusababisha fujo na uvunjifu wa amani mionganini mwa raia. Kwa msingi huu methali inaonya kwamba, si vyema kwa mtu awe mtumishi wa uma au mjasiriamali mwengine kutoa matusi au kuizungumza visivyo mamlaka inayotawala, kwani kufanya hivyo kunaweza kumsababishia matatizo baada ya harakati za uchaguzi kumalizika katika nchi au jamii anayoishi.

Kupitia nadharia ya Mwitiko wa Msomaji inayompa fursa mtafiti kuhakiki kazi ya fasihi kwa uzoefu na maono yake, katika uzoefu wakemtafiti amebaini kuwa katika jamii wapo baadhi ya watendaji wa serikali ambao hujihusisha na maswala ya kisiasa na kuidharau serikali iliyopo madarakani kwa kisingizio tu cha kwamba demokrasia

inawaruhusu kufanya hivyo huku wakisahau kuwa wao hawapaswi kujingiza katika wimbi hilo kwa sasa kwani suala hilo lina wahusika wake ambao wangepaswa kujihusisha nalo ambao ni taasisi na waajiriwa wa vyama husika. Kwa mfano, Baadhi ya watendaji wakuu na hata watendaji wa kawaida hujiungana na vyama vyu upinzani na kutoa maoni yao kwa lugha ya ukali na ufedhuli dhidi ya serikali yao iliyopo madarakani

Saba, mtafiti wa kazi hii amechambua methali isemayo kwamba “*Papa akipea Mafuta humpa Mwanawe*”. Methali hii hutumika kuonyesha namna watu wenye hadhi wanavyowarithisha watoto wao hadhi walizonazo. Msimbo wa kiishara wa Nadharia ya Simiotiki umetumika hapa kutumia neno mafuta kuwakilisha hadhi, cheo au kazi aliyonayo mzee. Huyo ni mzee ambaye hupenda kurithiwa na mwanawe kwa cheo, kazi au hadhi ya uongozi.

Katika uongozi methali hii inatumika sana kwenye nchi za Kifalme, ambako Mfalme anapofariki uongozi hupaswa kubebwa na mwanawe au mtu wa familia yake. Mafuta kwa mujibu wa nadharia tajwa ni ile hadhi ya ufalme ambayo hurithiwa na wanawe. Siyo nchi za Kifalme tu, bali hata katika nchi za kidemokrasia Tanzania ikiwemo, uongozi hurithiwa kutoka kizazi hadi kizazi.

Watoto wa watawala wa mwanzo, kama Abeid Amani Karume, Aboud Jumbe Mwinyi, Ali Hasaan Mwinyi na wengineo wameonekana kuchukuwa nafasi kubwa za uongozi au utendaji serikalini. Wapo waliowahi kuwa maraisi, kama alivyokuwa Amani Karume, wapo waliowahi kushika uwaziri, ubunge, uwakilishi wa nchi (ubalozi) na nyadhifa nyenginezo. Kwa mfano watoto wa mzee Ali Hassan Mwinyi,

wamekuwa katika nyakati tofauti wakishikilia nafasi mbalimbali za uongozi wan chi.

Wapo waliowahi kushika ubunge na uwaziri na hivi sasa pia mtoto mmoja wa Ali Hassan Mwinyi ni mgombea uraisi kwenye serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Kinadharia neno papa limetumika kumnasibisha papa na mwenye hadhi kupitia sifa ya utawala wa wawili hawa. Kiumbe Papa huwatawala viumbe bahari kama anavyotawala mtu mwenye hadhi kubwa wale walioko kwenye mamlaka yake.

4.3.5 Dhamira Vuate Ndani ya Methali zenyen Maudhui ya Kimapenzi

Kwanza, katika kipengele hiki mtafiti alichukuwa methali isemayo kwamba, “*Mambo kunga, n’vungu n’keka*”. Kwa mujibu wa BAKIZA neno ‘*kunga*’ lina maana ya siri za ndani. “*Mambo kunga*” hutumika zaidi kuhimiza umuhimu wa kuficha siri zinazotokea baina ya wana ndoa. “*Nvungu n’keka*” hutumika kama msisitizo wa kuzificha siri ndani ya moyo kama yafichwavyo mambo mvunguni ndani ya nyumba. Nadharia ya Simiotiki kupitia msimbo wake wa kiseme imeweza kujichomoza na kunasibisha mambo mawili katika methali hii, kwanza *ni ‘kunga’* lemye kuashiria siri zinazotakiwa kuhifadhiwa sana ndani ya moyo ya wanandoa hao, kwani safari ya maisha kwa wanandoa inaweza kukumbwa na misukosuko, dharba, shida na dhiki za kila aina kiasi ambacho iwapo wanandoa hawataweza kuwa wavumilivu na wastahamilivu wakubwa wakaweza kupambana na wimbi kali linalowakabili katika maisha yao, basi upo uwezekano mkubwa kwa ndoa yao kuvunika.

Pili nadharia ya Simiotiki kupitia msimbo wake wa kiseme inaweza kutumika kunasibisha baina ya ibara ‘*Nvungu n’keka*’ na uvumilivu, subra na ustahamilivu wa

mtu alionao juu ya jambo fulani ambalo linamthakili. Mwanandoa analazimika kuwa na tabia ya uvumilivu kwa lengo la kuienzi na kuinusuru ndoa yake ili iweze kudumu zaidi. Hutakiwa kusitiri aibu na sisi za ndani kama wazee wa kale walivyowakivitandikia na kuvisitiri mivunguni vitu vyao vyta thamani.

Methali hii inawahimiza wanandoa kujitahidi sana kuficha siri zao za ndani ya mioyo na kuwa ndio wasuluuhishaji wa mwanzo wa matatizo yao kabla ya kuyapeleka kwengine kwa ajili ya kutafuta suluhisho. Pia wanapoyatoa nje baadhi ya mambo yao kwa ajili ya kutafuta suluhu wanapaswa wafuate taratibu zenyne kufaa ili kufikia muafaka. Hadhari isipochukuliwa, utoaji wa siri za ndani unaweza kupelekea maafa makubwa kiasi cha kuiteteresha au kuivunja ndoa kabisa. Hii ndiyo maana iliyokusudiwa kwenye methali isemayo “*Mambo kunga, n’vungu n’keka*”.

Pili, katika eneo hili mtafiti wa kazi hii amejishughulisha kuchambua methali isemayo “*usichezee kusi kwa tanga bovu*”. Methali hii hutumika kutoa tahadhari kwa wanajamii wanaojaribu kutekeleza mambo ambayo kwa udhahiri yanaashiria kutotoa tija kutokana na viashiria vinavyojitokeza tangu awali. Viashiria vyta kutokufanikiwa kupitia Nadharia ya Simiotiki kwenye msimbo wa kiseme vimenasibishwa na tanga bovu, kwa kuwa tanga la aina hiyo lina sifa ya kukifanya chombo kisifike salama, kama viashiria fulani vinavyokwamisha mafanikio au natija ya jambo likusudiwalo kufanywa. Kwa mfano, mwanamme anaetaka kuoa mwanamke msanii, mcheza filamu ambaye waigizaji wenzake ni wanaume, hatarajiwi kuishi nae kwa kuelewana kutokana na mazowe na tabia zake za kisanii. Ule utabiri wa jamii kwamba huenda asiwezane nae husemwa kifasihi kuwa ni

“*kuchezea kusi kwa tanga bovu*”. Kusi niupepo uvumao kati ya mwezi wa Machi hadi mwanzoni mwa mwezi wa Agast, utokao kusini kuele kaskazini.

Upopo huu unadasturi ya kuzuka ghafla na kuwaangamiza wasafiri na wavuvi wanaotumia bahari kwa kuwasokota nap engine hata kuwazamisha. Wanaoathirika zaidi ni wale wenye vyombo vidogo, hasa vilivyodhaifu na vyenye vifaa vibovu. Kwa mfano mashua, majahazi madau na vyombo vyengine vyenye matanga mabovu ndio wahanga wakubwa zaidi. Hivyo kupitia nadharia ya Simiotiki kupitia msimbo wake wa kiseme umemnasibisha kusi na uwezekano wa kuingia kwenye matatizo iwapo hali fulani yenye viashiria vya hatari haikuepukwa mapema. Kuoa mwanamke mwenye dalili ya matatizo zilizowazi ni sawa na kutweka kwa tanga bovu na chombo kukingiza katika safari ya kusi. Kukosoana na kuingia kwenye mkorogeko wa ndoa ni rahisi sana, kama ilivyo rahisi kuzama kwa chombo kilichotwekwa kwa tanga bovu. Methali hii inamuhimiza kijana awe wa kike au wa kiume kuchaguwa mwenza bora ili asije akazama kwenye bahari au dimbwi la maangamizi.

Tatu, mtafiti alijishulisha na kuchambua isemayo “*Ukitumiavyo kipeku na kijungo utakitumia vivyo*”. ‘*Kipeku*’ni kijungo kilichokonga ambacho kinaelekea kwenye uchakavu na ubovu. Ni ‘*kijungo*’ ambacho kwa uchakavu na ubovu wake kinaelekea kupoteza hadhi na thamani. Kazi kubwa ya kijungo kinakuwa ni kuhifadhi na kupepetea vitu hasa vya aina ya nafaka na hata jamii ya kunde. Uswahilini vitu mashuhuri vipepetwavyo kutumia ungo au kijungo ni mtama, mpunga, uwele, ngano nzima, chooko, kunde, mbarazi na vitu vyengine vya aina hiyo. Kijungo ni kifaa kama hicho ambacho ni kipyä na chenyé kuthaminiwa na kupewa hadhi kutokana na

upya wake. Bibi mmoja aitwae Asha Msema Bungala alipoulizwa na mtafiti juu ya matumizi ya methali hii alisema “*methali hii hutumika katika jamii kuwaonya wanaume wanaodharau wake wao wa zamani na kuwapendelea wake zao wapya ambao wamewaoa siku za karibuni. Badala ya kumwambia mtu kwamba, usimdhara mkeo wa zamani, kwa sababu umepata mke mpya, kwa tabia uliyonayo ya kudharau mke mkongwe, hata huyo mpya naye baada ya muda utamdhara kama ulivyomdhara mke mkongwe*”. ‘*Kipeku*’ imetumika kiishara kuwakilisha mke wa zamani na ‘*kijungo*’ nayo pia imetumika kiishara kuwakilisha mke mpya. Hii inatokana na nadharia ya Simiotiki kupitia msimbo wake wa kiishara. Methali hii inatoa wasia kwa waowaji wa mitala kufanya uadilifu kwa wake zao wa zamani na wapya, ili kuleta usawa na insafu miongoni mwa wanajamii walio chini ya usimamizi wao. Tabia ya kukosa uadilifu haifai na haipaswi kuwepo kabisa katika jamii.

Nne, mtafiti alishughulikia methali isemayo, “*Miti mingine hayendwa yachana nguo mikekewa*”. ‘*Mikekewa*’ ni aina ya miti ambayo inadesturi ya kumchinja mtu mithili ya kisu kichinjavyo mwili wa mwanaadamu. Miti hii pia ikinasa nguo huichana wakati nguo iko kwenye mwili wa mtu anayetembea kwenye aina hii ya miti. Methali hii kwa mujibu wa bi Asha Hassan Hamad aliyejohiana na mtafiti siku ya tarehe 04-06-2021 huko Utaani, Wilaya ya Wete, kisiwani Pemba. “*Methali hii hutumika kutoa tahadhari kwenye maswali ya ndoa, kwa kumkataza kijana kuoa kwenye koo fulani ambazo zinasemwa kuwa na tabia ngumu zisizovumilika katika jamii*”. Nadharia ya Simiotiki kupitia msimbo wake wa kiseme imetumika hapa kunasibisha tabia mbovu za baadhi ya wanawake na tabia za mikekewa. Mikekewa huchana nguo na kuchinja mwili, kama vile ambavyo tabia mbovu husababisha

maafa kwa mume, jamaa zake na pengine hata kwa mali ya mume. Malezi ya watoto kwa mwanamke wa aina hii pia yanakosa mwelekeo. Bwana Haji Makame Bakari alisisitiza kwa kumwambia mtarifi kuwa, badala ya kumwambia mtu usimuowe fulani kwa sababu ya tabia na desturi yke mbovu utamwambia kwamba mwanangu jihadhari “*Miti mingine hayendwa yachana nguo mikekewa*”. Miongoni mwa dhamira vuate zilizomo katika methali hii ni katazo la kutokuowa wanawake kuotka kwenye familia zenye historia mbovu, ili kuepuka matokeo ya baadae yanayohofiya kutokea kutokana na rikodi za ukoo huo.

Katika maswali ya ndoa kuna kitu kinachoitwa kufu. Kufu ni kuo a mke au kuolewa na mume ambae ana ulinganifu wa tabia na muoaji au muolewa. Kuoa mke ambae kitabia halingani na muoaji au kuolewa na mume asiyelingana na muolewaji huweza kuleta mtarafuku mkubwa katika ndoa. Mtu hutakiwa aende panapoendeka na asiende popote, kwani “*Miti mingine hayendwa yachana nguo mikekewa*”.

Tano, mtarifi wa kazi hii alichambua methali isemayo “*Jifya moja halinjiki chungu*”. Jifya ni jiwe, tofali au pembe moja miongoni mwa pembe tatu zitumikazo kutengeneza jiko la kutelekea chungu au sufuria. Vifaa vya kutelekea chungu au sufuria jikoni ni lazima viwe vitatu. Kimoja au viwili havitoshi kukidhi hitaji la kuteleka sufuria au chungu. Kimatumizi methali hii haitumiki hivyo. Kwa bahati mbaya sana mtarifi alipohojiana na watafitiwa wake, walimueleza kwamba methali hii katika jamii zetu haitumiki vizuri. Huitumia watu wanaoamini kwamba mwanamke hawezi kuishi bila ya tendo la zinaa. Watu hawa wanaoamini kwamba mwanamke kuishi peke yake na mumewe haitoshi. Kwa mtazamo wao, mwanamke anatakiwa aishi na mumewe lakini pia furasa ya tendo la ndoa mara moja moja

anaweza kulifanya na mtu asiyekuwa mumewe. Kwaao wao mume mmoja hamtoshelezi mwanamke, kwani “*Jifya moja halinjiki chungu*”.

Methali hii hata hivyo, kwa mujibu wa babu Khatib Mjaka Ali “*ikitumiwa kwa maslahi ya kimaendeleo pia inaweza kuwa na muktadha bora pia. Methali hii inaweza kulingana na methali nyengine kama vile kidole kimoja hakivunji chawa, umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu*”, “*jicho moja halioni mwezi*”. Kwa muktadha mwengine tunaweza kusema kwamba, methali hii na nyengine kama hizi huweza kuvuata maana za kimuktadha na kuweza kutumika vizuri au vibaya kutegemea nia ya mtumiaji na muktadha wa matumizi.

Sita, mtafiti wa kazi hii amechambua methali isemayo “*Ntu halindi bahari ipitayo kila chombo*”. Mtafiti wa kazi hii alifanya usaili wa kikundi akiwa na wazee watatu wa Wawi, wenye umri wa utu uzima. Wazee hawa walisema kuwa ‘*methali hii inaenda sambamba na ule usemi usemao nke halindwa. Methali hii hutumika kukataza na kuwaasa watu wenye wivu wa kupindukia kutokana na desturi yao ya kufanya kile wanachoamini kuwa ni kuwalinda wake zao ili wasichukuliwe na wanaume wengine. Wazee hawa waliendelea kusisitiza kwamba Mwanamke akiwa kakusudia ukorofii hakuna namna yakulindwa. Alindwe au asilindwe akitaka kuzini atazini tu. Kwa hivyo mwanamke hulindwa kwa kutunzwa, kufunzwa maadili mema na kutoshelezwa haja zake huko nyumbani*’. Mtfaiti alipouliza bahari hasa inawakilisha nini katika methali hii, aliambiwa ‘*bahari ni mwanamke Malaya, asiyerudisha mkono wa mwanamme yoyote mwenye haja ya kugusu mwili wake*’. Dhana hii na mtazamo huu unaendana vyema na Nadharia ya Simiotiki kuitia msimbo wake wa kiseme ambao hujihusisha na vinasbishi vyaa kisemantikia kwa

kuangalia sifa bainifu za vitu viwili. Kwa mfano ‘*bahari*’ katika muktadha huu imenasibishwa na mwanamke malaya na ‘*chombo*’ inawezakana kunasibishwa na wanaume wahasharati waliojikita kwenye utashi wa zinaa na mambo yanayohusiana na jambo hilo. Mwanamke Malaya alinasibishwa na bahari, kwa kuwa bahari haichagui aina ya chombo cha kuelea ndani yake, kama mwana mke malaya asivyochagua mwanammme wa kutembea nae. Mwanamme muhasharati amefananishwa na chombo kwa tabia yake ya kuelea baharini ambako kumeakisiwa na mwana mke Malaya.

Saba, mtafiti amejishughulisha na uchambuzi wa methali ya Kipemba isemayo ‘*Tonga si Tuwi*’. Kwa mujibu wa BAKIZA (2010), tonga ni nazi yenye umbo kubwa sana umbo ambalo ni tafauti na nazi nyengine. Tuwi ni maji mithili ya maziwa yanayotokana na nazi iliyokunwa na kuchujwa. Kimantiki inatarajiwa nazi yenye umbo kubwa kwa mtazamo wa nje ndio inayotarajiwa kutoa tui jingi zaidi. Hata hivyo jambo hili mara nyengine linatokea kinyume na mambo yalivyo. Linaweza kujitokeza nazi kubwa kwa maumbile lakini kwa sababu moja au nyengine lisiwe na tui la kutosha licha ya ukbwa lilionao. Kwa kweli huu ni mtazamo wa juu juu uliotolewa kutockana na tafsiri ya vijenzi vya maneno viliyojenga methali wenyewe. Kimatumizi methali hii hutumika kuonyesha kwamba, muonekano wa nje siyo vyema kutumika kama kigezo cha kuchagua na kuridhika na kitu. Kiuhalsia methali hii hutumika kuonyesha hasara za kuteuwa wachumba kutegemea wasifu wa nje. Huweza kutokea mwanamke aliyekamilika umbo kwa uzuri na ujamilifu, mwenye sifa zote za uzuri wa mwanamke, lakini akawa na tabia dhaifu na chafu kupindukia. Kutockana na sifa na tabia zake mbovu, akawa haoleki na kumuowa mtu kama huyo

ikawa sawa na kuijiangamiza na kujitia shimoni. Utonga na tui ni viashiria viwili vinavyoashiria wasifu wan je na wandani. Wasifu wan je unaweza kuvutia sana ila mvuto wake si lazima uathiri wasifu wa ndani. Hii ni kwa mujibu wa Nadharia ya Simiotiki kupitia msimbo wake wa kiishara unaohusu usomaji na uhakiki wa kazi za kifasihi. Msimbo huu unahuishwa na jinsi ambavyo wasomaji wanaovumbua maana ya kiishara katika kazi za kifasihi.

4.3.6 Dhamira Vuate Ndani ya Methali zenyenye Maudhui ya Utamaduni

Kwanza, katika kipengele hiki mtafiti alichukuwa methali isemayo kwamba, “*ndege wa uta hafugwa*”. Uta ni aina ya mtego utengenezwao kwa mti wenyewe uwezo wa kupinda bila kukatika. Mtego wa aina hii hutegwa mithili ya mfyuka na hutumika kunasa ndege au wanyama pori. Wanyama au ndege wa aina hii hutegwa na kunaswa kwa ajili ya kutumiwa kwemye ulaji hasa kwa lengo la kitoweo. Wanyama hawa hawafugwi kutokana na ugumu wao wa kukubali kuishi chini ya himaya na uangalizi wa binaadamu. Ndege na wanyama wa aina hii hawafugiki na ndio maana Waswahili wakaibuka na methali isemayo “*ndege wa uta hafugwa*”.

Kimatumizi methali hii hutumika kuonyesha asiyesarifika kitabia na asiyekubali kuelekezwa na watu wengine. Tabia yake inakuwa chafu kiasi cha kutoweza kuishi na watu wengine. Ukumlazimisha kuishi kibinaadamu katika jamii, anaweza kuzuwa mtafaruku. Mtu wa aina hii hufananishwa na ndege wa uta kwa kuwa ndege wa aina hii hawezi kufugika na kuwazowea watu kama vile walivyo ndege wa aina kama ya bata, kuku, kanga na ndege wengine wafugwao kwenye jamii. Mtu huyu tabia yake ya kutokalika imefananishwa na ndege wa uta kutokana na tabia ya kutofugika. Mfanano huu ni kupitia Nadharia ya Simiotiki kwenye msimbo wake wa kiseme.

Pili, katika kipengele hiki mtafiti aliangazia na kuchambua methali isemayo kwamba, “*Msiwakwe yuna Mungu*”. Ni methali ya Kiswahili inayotumika kupinga upendeleo unaojitokeza katika jamii. Katika jamii zetu kama tujuwavyo kuna tabia ya upendeleo itokanayo na kujuana au ichochewayo na rushwa. Utakuta huduma kwenye jamii zetu hutolewa kupitia uenyeji au kutegemeana na rushwa za kimali au hata kungono. Kila mmoja anakuwa na mtu wake anaemtegemea kumtekelezea shida yake. Wapo wengine hujikuta wanakosa huduma za kijamii kwa kukosa uenyeji au kutotoa rushwa. Wanapolaamu upendeleo uliopo na kujutia kukosa kwaohuduma kwa sababu ya kutokuwa na uenyeji hujiegemeza kwa Mungu. Hujikuta wakiitamka methali hii kwa kusema *Msiwakwe yuna Mungu*”. Methali hii huonyesha ishara za kiimani na kukemea tabia ya kutoa huduma kwa kupendea.

Tatu, mtafiti amechambua methali ya Kipemba isemayo “*Nchelea ntoto wa shangazi hapati mwana*”. ‘Chelea’ katika Kipemba ni neno linalotumika lenye maana ya ogopa au hofia. Katika utamaduni wa Kiswahili, hasa katika siku za nyuma ilikuwa ni fakhari kubwa watu kuozeshana watoto wao kuzingatia uhusiano wao wa kidugu. Uhushiano uliopewa hadhi zaidi ni ule wa kuozeshwa watoto wa shangazi kwa mjomba. Baada ya waonaje wa aina hii baada ya kufunga ndoa uhushiano unaotambulika zaidi baina yao ni wa mke na mume. Uhushiano wa kidugu uliopo baina yao hufunikwa na ule wa ndoa. Hawastahiani kidugu, bali huheshimiana kindoa kama mke na mume. Methali hii hutumika kutoa tahadhari kwa watu wenye kuona muhali kuchukua hatua juu ya tukio la hatari linalohusisha ndugu wa damu. Methali inawataka wanajamii kuchukua hatua dhidi ya kosa au uovu uliotendeka bila kujali uhushiano wa damu. Kinachoziingatiwa ni kanuni na sheria zilizowekwa.

Mchukua hatua akichelea uhusiano wa damu katika utekelezaji wa sheria, malengo huenda yasifikasiwe.

Nne, mtafiti amechambua methali ya Kipemba isemayo “Kimbia Ugwe Kabla hujaona Ng’ombe”. ‘Ugwe’ni neno linalotumika Pembra likiwa na maana ya kamba katika Kiswahili Sanifu. Kamba za aina hiyo hutumiwa na wachungaji hasa wa ng’ombe kwa ajili ya kudhibiti wanyama wao. Maana ya dhahiri iliyotokana na vijenzi vyta methali hii sivyo hasa vilivyokusudiwa kuwasilishwa na methali hii kifasihi. Methali hii imewasilishwa kiishara kuakisi maafa yanayoweza kutokea na dalili zake za awali. ‘Kamba’ ni kiashiria kinachowakilisha dalili za awali za uwezekano wa kutokea kwa maafa na ng’ombe ndiyo maafa wenyewe. Hii ni kutokana na Nadharia ya Simiotiki kupitia msimbo wake wa kiishara unaohusishwa na jinsi ambavyo wasomaji wanavyovumbua maana ya kiishara katika kazi za kifasihi.

Wanajamii wanatakiwa kupitia mafunzo ya methali hii kuelewa kwamba kinga ni bora kuliko tiba. Wanatakiwa wachukue tahadhari ya kujikinga na maafa yanayokwishatabiriwa. Mamlaka ya hali ya hewa kwa mfano inapotangaza utabiri kuja kwa mvua kubwa, upepo na kimbunga ni wajibu wa raia ni kuchukua tahadhari mapema kabla ya kutokea kwa maafa wenyewe. Utabiri huu unakuwa ni kuona kamba, ambao katika methali hii umejulikana kuwa ni “ugwe”. Kamba hii inapaswa kukimbiwa kwa juhudini na jitihada kubwa. Ng’ombe anapowasili huleta maafa makubwa iwapo hatokimbiwa katika hatua za mwanzo pale kamba inapoonekana katika hatua za awali.

Tano, mtafiti wa kazi hii kwenye kipengele hiki cha utamaduni amejihuisha na methali isemayo *Ndoa ncutia nkono kizani*. Kutia mkono kizani ni tendo la kubahatisha. Inawzekana kubahatika na kuokota kitu bora na chenye thamani kubwa. Kwa kuwa mtu hana uhakika juu ya akiokotacho anaweza pia kupata hasara na maafa ya kutafunwa na mdudu hatari kama nyoka, nge au hata tandu kwa kupeleka kwake mkono mahali pasipo mwangaza.

Methali hii inaweza kuibuka na dhamira nyingi vuate. Dhamira iliyodhahiri ni ya ndoa. Kwa hakika mtu yoyote anayeoau kuolewa huwa hana uhakika wa ustawi wa ndoa yake. Ndoa yake inaweza kunyooka na kupata mafanikio kwenye maisha. Lakini wakati mwengine ndoa inaweza kukumbwa na mtafaruku na kuleta matokeo hasi. Ile hali ya kutokujua kipi kitatokea katika maisha ya ndoa kimefananishwa na tendo la kutia mkono kizani. Hili inaakisi kabisa nadharia ya Simiotiki kupitia msimbo kiseme unaweza kunasibisha elementi mbili za kisemantiki. Uhusuano huu unaonyesha kwamba ndoa ni kbahatisha, sawa na abahatishavyo mtia mkono kizani. Anaweza kupata kizuri au akapata kibaya. Hali hii inafanana na mwana ndoa ambaye aidha hufanikiwa akaishi maisha ya raha au huharibikiwa akaishi maisha ya karaha.

4.4 Hitimisho

Kwa ujumla sura hii ya nne ilichambua na kudadavua data za utafiti zilizokusanywa uwandani na maktabani. Katika uchambuzi wake mtafiti alibaini kwamba methali za Kipemba zimevuata dhamira an'wai zinasoakisi hali ya maisha ya wakaazi wa Pemba na mazingira yao. Miongoni mwa dhamira zilichambuliwa ni zile zilizohusu mambo ya kijamii, shughuli za kisiasa, harakati za kimpenzi na hata sekta za mila na tamaduni za jamii.

SURA YA TANO

MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi

Hii ni sura ya tano na ya mwisho katika utafiti huu. Sura hii ina sehemu tatu. Sehemu ya kwanza ni ile inayowasilisha muhtasari wa tasnifu nzima ya utafiti huu. Sehemu ya pili imetumika kuonesha hitimisho la utafiti ambapo pamoja na mambo mengine matokeo ya utafiti huu yanajitokeza kwenye sehemu hii na sehemu ya tatu inatoa mapendekezo ya utafiti huu.

5.2 Muhutasari wa Tasnifu

Utafiti huu ulikuwa na lengo la kuchunguza dhamira Vuate zinazoibuka katika Methali za Kipemba. Utafiti huu ulikuwa na malengo mahususi mawili. Lengo la kwanza lilikuwa ni; “Kubainisha Methali Mahususi za Jamii ya Kipemba.” Lengo hili liliongozwa na swali la utafiti lisemalo, “Ni methali zipi mahususi za jamii ya Kipemba?” Lengo mahususi la pili lilikuwa ni “Kubainisha Dhamira Vuate zinazojitokeza katika Methali za Jamii ya Wapemba. Lengo hili liliongozwa na swali la utafiti lisemalo “Ni Dhamira zipi zinazovuatwa katika Methali za Jamii ya Wapemba”?

Tasnifu hii ina jumla ya sura tano. Sura ya Kwanza ni sura ya utangulizi ambayo inaeleza mambo ya msingi yanayohusu utafiti huu. Katika sura hii mtafiti amebainisha na kueleza usuli wa mada ya utafiti, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti na muundo wa tasnifu.

Sura ya pili inahusu mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa Nadharia. Sura hii ina sehemu ya utangulizi, Sura hii pia imechunguza dhana muhimu katika utafiti huu ambazo ni pamoja na ufanuzi wa dhana kuhusu methali, lugha katika methali, dhana ya dhamira, dhana ya fasihi, mapitio ya maandiko kuhusu methali pamoja na pengo la utafiti. Mwisho sura hii imeelezwa Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji pamoja na Nadharia ya Simiotiki zilizotumika katika uchambuzi wa kazi hii. Katika sura ya tatu, utafiti huu umeelezea kuhusu mbinu za utafiti. Vipengele vilivyoelezwa katika sura hii ni utangulizi wa sura, eneo la utafiti, kundi lengwa, sampuli na usampulishaji, ukusanyaji wa data ambapo kipengele cha data za msingi na data za upili kimefafanuliwa. Vipengele vyengine viliyooneshwa katika sura hii nimbinu za kukusanya data, ambapo mbinu za hojaji na mahojiano zilitumika. Mwisho kabisa, kipengele cha usahihi wa data, kuaminika na maadili ya utafiti vilichambuliwa.

Sura ya nne imefanya uchambuzi na uwasilishaji wa data za utafiti huu. Sura hii imegawanyika katika sehemu ndogo ndogo mbili. Sehemu hizo zimepangwa kutegemeana na malengo ya utafiti huu. Sehemu ya kwanza iliwasilisha data za utafiti zinazohusu lengo la kwanza. Sehemu ya pili ni uwasilishaji wa data za utafiti zilizohusu lengo la pili. Sura ya tano imehitimisha kwa kutoa muhtasari wa utafiti, hitimisho na mapendekezo. Sura hii inaeleza kwa muhtasari kile kilichogunduliwa na matafiti. Maswali yote mawili yaliyoongoza utafiti huu yametolewa majibu yake kwa ufupi kama ilivyobainishwa na kugunduliwa katika sura ya nne ya tasnifu hii. Hivyo basi, matokeo ya utafiti huu yalikuwa kama ifuatavyo:

5.3 Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu ulikuwa na malengo mawili ya utafiti. Kukamilika kwa utafiti huu kumetupa matokeo kama yafuatayo:

5.3.1 Lengo Mahususi la Kwanza

Lengo mahususi la kwanza la Utafiti huu lilikuwa ni: “Kubainisha methali mahususi za jamii ya Wapemba.” Lengo hili liliongozwa na swal la utafiti lisemalo “Ni zipi methali mahususi zinazopatikana katika jamii ya Wapemba?”

Matokeo ya utafiti huu yalionesha kuwa methali za jamii ya Wapemba hujitokeza katika katagoria na makundi mbalimbali. Zipo zile zinazohusu maswali ya kijamii, kiuchumi, kisiasa, kimpenzi na hata kiutamaduni. Mtafiti aliziorodhesha methali kadha zilizo katika kila kundi kutegemeana na katagoria yake iliyohusika.

5.3.2 Lengo Mahsusisi la Pili

Lengo mahsusisi la pili la utafiti huu lilikuwa ni: “Kubainisha dhamira vuatu zilizojitokeza katika methali za jamii ya Wapemba.” Lengo hili liliongozwa na swal la utafiti lisemalo “Ni dhamira zipi zilizovuatwa katika methali za jamii ya Wapemba?” Matokeo ya utafiti huu yalipatikana kwa kuchambua methali saba kutoka kila kundi na dhamira mbalimbali zilivuatwa kutoka kila methali. Zipo methali zilizovuata dhamira moja na nyengine kujitokeza kuvuata dhamira zaidi ya moja. Baadhi ya methali za kundi fulani huvuata dhamira zilizo kwenye kundi lake na kuchupa mipaka kuvuata dhamira zilizo kwenye makundi mengine pia.

Kwa ujumla dhamira zilizovuatwa zilihusu, malezi, biashara, uvuvi, usafiri, mambo ya shughuli za kijamii kama maziko, harusi, uhusiano baina ya watu, mambo ya siasa, utamaduni,

5.4 Hitimisho

Utafiti huu ulilenga kuchunguza dhamira vuate zinazojitokeza katika mehali za jamii ya Wapemba. Methali za jamii ya Wapemba zimevuata dhamira mbalimbali zilizozagaa katika Nyanja mbalimbali za kijamii. Dhamira hizi zilizovuatwa na methali ni zenye manufaa makubwa mno katika kuilea na kuielekeza jamii ya watu wa Pemba, kama tanzu nyengine za fasihi simulizi zinavyobeba jukumu linalolingana na hili.

5.5 Mapendekezo ya Utafiti

Kukamilika kwa utafiti huu ni wazi kuwa kumeleta faida kwa jamii na kuonesha maeneo muhimu yanayohitaji kufanyiwa kazi. Hivyo utafiti huu unapendekeza yafuatayo:

5.5.1 Mapendekezo kwa Watafiti

Kwa watafiti wasomi wanaotegemewa na Taifa, ni jukumu lao kufanya tafiti zaidi, juu ya tanzu tofauti za fasihi ili kuzidi kufichuwa maarifa yaliyofumbatwa kwenye fasihi hiyo. Mtafiti anapendekeza kufanyika utafiti linganishi unaolinganisha methali za Kiswahili Sanifu na methali za lahaja mbalimbali za lugha hii. Pia mtafiti anapendekeza kufanyika utafiti linganishwa fani na maudhui kati ya methali za Kiswahili na methali za lugha nyengine za makabila ya Tanzania. Methali za

Kiswahili zinaweza kuibuliwa kutoka katika Kiswahili Sanifu au hata kutoka katika lahaja za lugha hii.

5.5.2 Mapendekezo kwaWakuza Mitaala

Mtafiti wa kazi hii anawashauri wakuza mitaala wa taifa kuingiza katika mitaala ya Kiswahili mada zinazozungumzia methali za lahaja mbalimbali, badala ya kujikita katika methali za Kiswahili Sanifu peke yake.

5.5.3 Mapendekezo kwa Waandishi wa Vitabu

Mtafiti anawashauri waandishi wa vitabu na watunzi wa makamusi, kuandika makamusi ya methali za lahaja za Kiswahili kama vile ya Kiswahili Sanifu ilioandikwa na Wamitila (2004). Mtafiti anashauri pia methali za Kipemba zikusanywe kama vile alivyozikusanya Mauya (2006).

MAREJELEO

Adam, J. & Kamuzora, F. (2008). *Research Methods for Business and social studies.*

Mzumbe Book Project, Morogoro, Tanzania.

Ali, K. H. (2018). Dhima ya Majina katika Vyombo vya Uvuvi kwa Jamii ya Watumbatu. Tasnifu ya Uzamili MA-Kiswahili katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Alhabib, E. (2012). *Matumizi ya Lugha katika Nyimbo za Taarab.* Tasnifu ya M.A Kiswahili Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Bwanamaya, B. J. (2004), “Uhusiano Kati ya Methali na Mabadiliko Katika Jamii.” Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam, Tanzania.

Enon, J.C (1998). *Educational Research; Statistics and Measurement.* Kampala: Makerere University Press.

Chacha, P. E. (1999). Endangered African Proverbs Collections: Kurya (Kenya, Tanzania) Proverbs, Musoma: Contribution of The African Proverbs Project.

Fadhil, F. E. (2014). *Kuchunguza Dhima ya Mtindo katika Tamthiliya za Historia: UtafitiLinganishi wa Tamthiliya za Morani na Kinjeketile.* Tasnifu ya Uzamli MA-Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Faki, M. H. (2018). Matumizi ya Lugha Tandawazi katiaka Mitandao ya Kijamii: Changamoto katika Lugha ya Kiswahili. Tasnifu ya Uzamli MA-Kiswahili katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Gaichu, M. N. (2016). *Kuchunuza Sitiari Dhanfu Katika Methali za Kiswahili-Mtazamo waNadharia ya Uhusiano*. Tsnifu ya Uzamili ya MA-Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Nairibi.

Gaspar, I. C. (2012). *Methali, Nahau, Vitendawili na Mafumbo*. Dar es Salam: Khashu Investment

Hassan, H. A. (2017). *Kuchunguza Fasihi ya Majina ya Mitaa Mjini Unguja*. Tasnifu ya Uzamili MA-Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Jilala, H. (2016). *Misingi ya Fasihi Linganishi*. Dar es Salam: Daud Publishing company

Julia, W. (2013). *Kanga kama Salijili Maalumu ya Kisanii na Mawsiliano*. Tasnifu ya UzamiliMA-Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Moi.

Juma, A. R. (20150. *Methali za Kswahili ilizoachwa: Sababu na Athai zake kwa Jamii*. Tasnifuya Uzamili MA-Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Dodoma

Kahmis, S. A. M. (1983). *Nafasi ya Fasihi Simulizi katika Jamii ya Tanzania*. Katika Jarida la Mulika Na. 15 uk. 3-13.

Khatib, T. O. (2017). *Dhamira Zijengwazo na Taswira katika Methali za Wapemba*. Tasnifu yaUzamili MA-Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar.

Kipacha, A. (2014). Misemo katika Lugha za Magari: Divai Mpya? Katika Jarida la Swahili Forum Na. 21, uk. 104-121.

- Kombo, D. K & Tromp, D. L. (2006). *Proposal and thesis Writing. An Introduction.* Nairobi: Paulines Publications Africa.
- Kothari, C. R. (2008). *ResearchMethodology; Methods and Techniques.* New Delhi: New Age. International Publishing Limited.
- Madumulla, J. S. (2005). *Proverb and Saying: Theory and Practice,* Dar es Salaam: University Press. Dar es Salaam: Institute of Kiswahili Research.
- Maitaria, J. N. (2012). Uainishaji wa Ushairi wa Kiswahili kwa Kutumia Kigezo cha Methali. Katika Mulika Na. 31, uk. 89-104.
- Mahenge, P. (2009). Semi zitumikazo kwenye tiketi za daladala, *Mulika* Na 29 na 30. TATAKI.
- Massamba, M. (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha.* Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.
- Masebo, J.A. & N. Nyangwine,(2008). *Nadharia ya Fasihi [M],* Dar es Salaam: Nyambari Nyangwine Publishers
- Matteru, May L. N. Balisidya (2003), *Nadharia ya Fasihi Simulizi [R],* Dar es Salaam: Semina ya Fasihi Simulizi, TUKI,.
- Mauya, A. B. (2006), *Semi Maana na Matumizi [M],*: TUKI, Dar es Salaam
- Migpdela, W. (2017). *Dhamra za Maandishi ya Kuta za Vyooni Jijini* Dar es Salam.Katika Jarida la Mkwawa Journala of Education Na. 1 uk. 1-8.

Mmbaga, N. O. (1978). *Dima ya Ushairi katika Kuhifadhi Historia ya Lugha*. Katika Jarida laMulika Na. 14, uk. 19-26.

Mtesigwa, G. K. (2013). *Kuchunguza Matumizi ya Methali katika Jamii ya Wanyiramba*. Tasnifu ya Uzamili MA-Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Tanzania.

Mulokozi, M. M. (1989). *Tanzu za Fasihi Simulizi*. Mulika 21:1-24, Dar es Salaam: TUKI.

Nkwera, F.V.(1999) *Tamrini za Fasihi Simulizi* [M], Dar es Salaam: Business Printers Limited. (1996). *Fasihi ya Kiswahili* Chuo Kikuu Huria Cha Dar – es-Salamu.

Msuya, P. A. (1977). *Fasili ya Methali*. Katika Jarida la Mulika, Na. 9 uk. 29-31

Mwenerwa, J. (2003). “Methali za Jamii ya Wahaya wa Mkoani Kagera,” Tasinifu Ndogo ya Shahada ya Kwanza, Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

Nassor, H. J. (2016). *Semi Zilizoandikwa Kwenye Vyombo vya Safari vya Baharini Kisiwani Pemba*. Tasnifu ya Uzamili MA-Kiswahili katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Ndungo, C. W. na Mwai, W. (1991). *Kiswahili Studies: Part Two*. Nairobi: University of Nairobi

Ndungo, C. M. & Waful, R. M. (1993). *Tanzu za Fasihi Simulizi*. University of Nairobi.

Njogu, K. na Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu.*

Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Panneerselvam, R. (2012). *Research Methodology*. New Delhi: PHI Learning Private Limited

Sengo T.S.Y.M. (2009). *Sengo na fasihi za kinchi*. Dar es Salaam: AERA Kiswahiki Research Products

Senzighe, R. (2004). “Usawiri wa Mwanamke Katika Methali za Wapare,” Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam.

Skuni, M. M. (2018). *Kuchunguza Jinsi Nahau za Kiswahili Sanifu Zinavyokwamisha Mawasiliano Fanisi kwa Wageni wa Lughu*. Tasnifu ya Uzamili MA-Kiswahili katika chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Taasisi ya Ukuzaji Mitaala (1988). *Kiswahili Sekondari*. Dar es Salaam: TUMI.

Timothy, K. M. (2016). *Maana ya Usemi na Mazungumzo katika Mitandao ya Kijamii Hususan Facebook na Twetter*. Tasnifu ya Uzamili MA-Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Nairobi.

Walliman, N. (2011). *Research Methods*. London: Routledge.

Mulokozi, M. M. (1989). *Tanzu za Fasihi Simulizi, Mulika 21,1-24*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Wafula, R. M. (1999). Uhakiki wa Tamthiliya Historia na Maendeleo yake. Nairobi: Jomokenyatta Foundation

Wafula, R. M. na Njogu, K. (2007). Nadharia za Uhakiki wa Fasihi. Nairobi: Jomokenyatta Foundation.

Wamitila, K. W. (2002). *Misingi ya Nadharia ya Fasihi*. (Chapa ya Pli). Nairobi: Video Muwa Publications Ltd.

_____ (2010). *Kanzi ya Fasihi 1: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide Muwa Publications Ltd.

_____ (2013). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Publications Ltd.